Hii Ndiyo Ishara Ya Mwisho, Bwana?

Asante sana Ndugu Neville.

Habari za jioni, rafiki zangu wapenzi. Basi. Ndiyo. Hilo ni zuri. Ninayo furaha sana kurudi tena usiku wa leo katika utumishi wa Bwana, Mungu wetu. Niliwacheleweshа sana asubuhi hii mpaka najisikia kama yanibidi niharakishe sana usiku wa leo. Jamani, lilikuwa jambo baya sana kusimama, na ni baya jinsi ile ile usiku wa leo. Na kwa hiyo, haitachukua muda mrefu mpaka tutakapokuwa na nafasi kwa ajili yenu, mnaona, mara tu kanisa limalizikapo.

La, lakini hatupangi kukaa muda mrefu sana usiku wa leo. Ila kesho usiku, tunakusudia kukaa kwa muda kidogo. Kesho usiku, iwapo baadhi yenu mwaweza kuja kesho jioni, mbona, tunatarajia kuwa na wakati mzuri katika Bwana. Watakuwepo baadhi ya watu wazuri hapa kesho usiku . . . Tutakuwa . . . sote sisi tuna wakati . . . Tutashiriki meza ya Bwana usiku wa manane kesho usiku. Nina hakika mtapenda kuwa na . . . kuja kwa ajili ya hilo. Wakati ambapo wengine wanapiga makelele, vifijo, wakipiga bunduki, wakinywa, na kadhalika, tutainama tu kwa kicho mbele za Mungu na kushiriki meza ya Bwana, na kuanza mwaka kwa ahadi yetu . . . mioyo yetu kwa Mungu katika kujitoa Kwake.

Pia patakuwa na wahubiri wazuri hapa kesho usiku, hapana shaka. Kuna baadhi ya . . . ndugu toka Georgia yupo hapa—Ndugu Palmer, mhubiri wa ajabu. Ndugu Junior Jackson atakuwepo hapa kesho usiku—Ndugu Beeler, Ndugu Neville. Loo jamani, jamani! Na kuendelea na kuendelea. Mtu mzuri wa Mungu atakuwepo hapa. Ndugu Wilber Collins, na wote hao ndugu ambao wamekuwa wakitupa jumbe nzuri kama hizo; na labda wengine watawasili, kwa hiyo tutatarajia wakati mzuri kesho usiku.

Sasa mke wangu alisema, “Usiseme hili,” lakini yanibidi niliseme kwa vyo vyote. Nasikitika nilisema *Empire* asubuhi hii badala ya *umpire*. Billy akiketi nyuma kule alisema, “Huyoo!”

Nilisema, “Empire, yapaswa awe na empire.” Nilimaanisha *Umpire*. Niko kama walivyosema juu ya yule Mdachi, wajua—“Msinichukulie kwa ninachosema, lakini ninalomaanisha.” Kwa hiyo, nikasema, “Nafikiri wananielewa baada ya miaka yote hii.”

Wajua hii ni kama . . . hii ni miaka thelathini nimekuwa kwenye mimbara hii. Miaka thelathini katika maskani Hii.

Yawapasa muwe mumenijua wakati huu, sivyo? Loo jamani, elimu yangu hakika ni haba. Siwezi kuzungumza, lakini nampigia Bwana makelele ya kweli.

Ndugu, naamini ilikuwa Daktari Lamsa, ilikuwa yule wa Biblia ya Lamsa, katika tafsiri ambapo alisema . . . Wakati mmoja nilikuwa ninazungumza na sikujua alikuwepo. Akarudi na alikuwa akizungumzia kuhusu Urimu na Thumimu—kisha alikuwa akizungumzia kuhusu Nuru ile naye akasema, "Watu hawa wana nini siku hizi?" Nami nikasema, "Sababu watu, watafsiri, hawakuweza kufasiri Biblia sawasawa, ilikuwa kwamba watafsiri walijaribu kufasiri katika Kiyidi cha tabaka ya juu, na Yesu akizungumza, alizungumza kile cha tabaka ya watu wa kawaida, kama watu wa mitaani walivyozungumza." Na mnajua kuna Andiko katika Luka lililosema, "Watu wa kawaida walimsikiliza Yeye kwa furaha." Alizungumza katika lugha yao. Natumaini hivyo ndivyo ilivyo tena.

Tunafurahi kwa ajili ya Bwana. Sasa najua . . . Nawaona hao mabibi wamesimama kule . . . Ni vibaya vya kutosha kuwaona wanaume wakisimama, sembuse hao wasichana, wavulana, na mabibi, na kadhalika, wakisimama kwenye kuta—na watoto wadogo. Lakini hatuna nafasi ya kutosha kuketi, kwa hiyo tunaomba kwamba wakati mwingine tuwapo na mikutano, baada ya juma hili; baada ya muda huu . . . Unajua, kitu kinachofuata, kadiri tunavyojua, ni zile Muhuri Saba; na Bwana akipenda, tutazianza mara tu kanisa linapomalizika—kujengwa ili tuweze kuingia humu. Tunakuja kwa kujitoa mara nyingine, na labda mnamo juma moja hadi mawili, na labda mkutano wa wiki tatu mfululizo, sasa—kuja kwa zile Muhuri Saba. Hivyo, tunatazamia wakati mzuri sana katika Bwana wakati huo. Nasi tuta . . . Ninyi watu wote kutoka nje ya mji, tutawapelekeeni kadi na kila kitu mpate kujua wakati hasa, labda juma moja au mawili mapema.

Kondrakta, kama nilivyomwelewa Billy akisema usiku wa leo, atakuwa amekwisha maliza tarehe kumi Februari. Vema, kama amemaliza mnamo tarehe kumi, tutaanza mnamo tarehe kumi na tano basi. Hivyo mara tu wamalizapo, tutaanza moja kwa moja na hilo.

Dada mkongwe Kidd, alinipigia simu muda mfupi uliopita, huku nusura anatokwa na machozi. Akasema, "Ndugu Branham, tulijitahidi sana kutia moto lile gari kuukuu, nalo halikushika moto." Kwa hiyo akasema, "Wewe omba kwamba lishike moto, na nitakuja kesho." Kisha akasema, "Nashangaa kama nitapata mahali pa kukaa?"

Nikasema, "Usiwe na wasiwasi, tutakupatia chumba, Dada Kidd, mara tu ufikapo hapa."

Akasema, "Ubarikiwe." Akasema, "Wajua, kama utakuwa na ibada hadi saa sita, sitaki kutoka kwenye saa sita."

Unajua, yeye na Ndugu Kidd wana kama miaka themanini na mitano kila mmoja, na bado wangali katika huduma. Unajua wanafanya nini? Wana kinasasauti, na huchukua jumbe zangu na kuzuru hospitali kwa hospitali, nyumba kwa nyumba, wakicheza kanda. Sasa, kama hilo si, si kustaafu—huko si kustaafu kazi. Huko ni kushikilia imani hadi mwisho, kufa umeshika Upanga mkononi. Hiyo ndiyo jinsi ya kwenda. Hivyo ndivyo ninavyotaka kufanya.

Kisha basi akasema, "Unajua, kama nikiingia kwenye barabara kuu kwenye saa sita, akasema, na baada ya saa sita za usiku, nikijaribu kufika nyumbani, na pepo hao wote waliolewa, akasema, akasema, wakienda zao kasi, wakinywa—hao pepo wakiendesha kasi huku na huko, nitaogopeshwa kupindukia."

Ndugu Pat, kwa hakika yeye yuko hivyo. Maskini jamaa huyo... Wangapi wanamjua Dada Kidd? Yeye huketi hapa, akionekana maskini mtawa.

Na wakati, hebu fikiri, miaka kadha kabla sijazaliwa (na mimi mzee) yeye alikuwepo juu huko kwenye milima ile—yeye na Ndugu Kidd. Angefua nguo siku nzima kwenye ubao wa kufulia ili kupata senti kumi na tano au ishirini kwa kufua kwake, apate kumpeleka mahali fulani usiku ule kuhubiri —kwenye hiyo migodi ya makaa juu kule Kentucky, ambapo ilibidi mtu fulani akulinde na bunduki upate kupanda kilimani ambapo ulienda kuhubiri. Loo, jamani! Basi nafikiri,

"Yanibidi nichukuliwe Mbinguni kwenye
kitanda cha anasa,
Wakati wengine walipiga vita wapate tuzo na
wakaabiri bahari ya damu?
Lazima nipigane kama nitatawala;
Ongezea uhodari wangu Bwana..."

Basi, ninataka msaada Wake kwa Neno Lake. Hilo ndilo ninalotaka usiku wa leo.

Sasa, nadhani vinasasauti vinafanya kazi sasa. Loo ndiyo—nasikitika Dada mdogo alikuwa na mtoto mchanga hapa asubuhi hii aliyetaka awekwe wakfu. Nami nilimwambia hakika tungelilitenda usiku huu. Na sasa, na kesho usiku tutawaweka wakfu watoto wachanga, ibada za uponyo, kila kitu ambacho twaweza kukitenda. Tunao muda wa kutosha...

Sasa, naenda kuwaomba fadhili kidogo vijana na matineja. Nami najua ni vigumu. Huwezi kusimama kimya kwa muda mrefu sana, kwa sababu miguu yako itapinda; lakini ninaliendea jambo fulani usiku wa leo ambalo sijawahi kulitenda mbeleni. Kuna jambo ambalo naenda kulizungumzia, ambalo sijawahi kufikiria kuzungumzia juu ya jambo kama hilo.

Hii ndiyo sababu, asubuhi hii, sikutaka kuweka wakati ule kabla ya ujumbe, nami kamwe sikuwahi kumaliza kuzungumzia

kuhusu *Yakini* yangu—nami sidhani nitawahi. Nataraji sitamaliza. Yeye ni wa ajabu sana.

Lakini usiku wa leo nitazungumzia juu ya jambo ambalo silijui. Sasa, hilo kweli ni jambo zito kwa mhudumu kusema: kwamba atazungumzia jambo ambalo halijui. Bali ninabahatisha, kwa fahamu zangu zote, ili kanisa hili liweze kuelewa. Nami nisingewaficha, kwa namna yo yote, kitu cho chote ambacho ni cha faida.

Na basi kanda hii . . . (Nadhani wavulana wanarekodi kanda) na kama ikitokea unapata hii kanda (ye yote ambaye anasikiliza kanda) kumbuka, kama jambo fulani linakutatiza, usiliseme isipokuwa lipo katika kanda! Usiseme kitu kinyume cha yaliyo katika kanda.

Wengi sana wananiandikia kuhusu *Uzao wa Nyoka* na kusema kwamba nilisema hivi na vile. Nami huenda nikachukua ile kanda na kuicheza yote—sikusema jambo hilo namna hiyo. Waona, watu wanaamua vibaya mambo.

Wajua, Yesu, wakati mmoja baada ya kufufuka Kwake, alikuwa akitembea chini ufukoni mwa bahari pamoja na mitume, na Yohana alikuwa ameegemea kifuani Mwake, nao wakasema, "Itakuwaje kwa mtu huyu?"

Yesu akasema, "Imekupasaje wewe ikiwa nataka huyu akae hata nijapo?" Basi neno hilo likaenea kwamba Yohana ataishi hata Yesu ajapo. Na Andiko lasema, "Walakini, Yeye kamwe hakulinena hilo jinsi hiyo."

Unaona, Yeye hakusema hilo kamwe. Yeye alisema tu, "Imekupasaje wewe ikiwa huyu atakaa hata nijapo?"

Hakusema kamwe angekaa, lakini unaona kuelewa vibaya—ni rahisi sana.

Sasa, si kwamba ninamlaumu mtu kwa kutenda hilo, kwa sababu mimi mwenyewe hulitenda. Na watu wote hulitenda. Kama mitume, waliotembea pamoja na Bwana wetu, walimuelewa Yeye vibaya—na kamwe hawakumuelewa vizuri . . . Mwishoni kabisa walisema, "Loo, sasa tunafahamu! Sasa tunaamini, nasi tuna hakika kwamba huna haja ya mtu akuambie Wewe kitu cho chote kwani Wewe unajua mambo yote."

Na Yesu akasema, "Mnaamini *sasa?* Unaona. Baada ya muda wote ule, hatimaye mna . . . hatimaye limewaelea, hata mkaamini?"

Na huo ni ubinadamu tu, na sisi sote tu binadamu. Kwa hiyo tutaelewa vibaya, lakini kama kwa namna fulani linakutatiza kidogo, cheza hiyo kanda tena. Sikiliza kwa makini basi. Sasa nina hakika Roho Mtakatifu atakufunulia.

Basi watoto wadogo, kama mtazuia amina zenu—watoto. Hebu ngojeeni kidogo, kwa sababu nataka hili hakika lieleweke,

sababu wengi hawatakuwa na kanda. Kwa hiyo, nawatakeni mhakikishe mnalielewa, na hebu tuliendee ningesema kwa dakika thelathini na tano au arobaini, kwa kicho sana tuwezavyo, kwa sababu jambo hili ni muhimu mno kwangu. Ni ambapo jambo fulani limetokea hata sijui la kufanya, mnaona. Nimo katika hali ngumu mno niliyowahi kuwa nayo, katika siku za huduma yangu, kama nijuavyo. Kwa hiyo hebu na tuinamishe vichwa vyetu, sasa, kabla ya kuliendea Neno.

Baba wa Mbinguni, basi hivi majuzi, nilihubiri juu ya somo la, *Kuthubutu*. Na *Kuthubutu* ni kubahatisha jambo bila idhini. Na labda usiku wa leo, Bwana, nimejichukulia kufasiri jambo fulani kwa watu bila ya kuwa na ono la jambo hilo. Kwa hiyo Bwana, nizuie ambapo haparuhusiwi. Fumba kinywa changu, Bwana. Wewe ulifumba kinywa cha simba wakiwa na Danieli katika tundu hata hawakumdhuru. Basi Bwana, naomba kwamba kama nikijaribu kufasiri jambo fulani vibaya, Wewe bado unao uwezo wa kufumba kinywa. Lakini kama ni kweli, basi, Bwana, ibariki, na uisambaze, na Wewe unajua hali na kile kinachokaribia. Hiyo ndiyo sababu naja, hata kwenye wakati huu wa mwisho kabisa, mimbarani kujaribu kufasiri mambo haya. Nami nakuomba Wewe utusaidie.

Bariki kanisa hili dogo. Kundi hili ambalo huja hapa chini ya dari hii, ambalo ni wageni wetu hapa mjini—wakitoka kwenye mikoa mingi. Loo, wakati vivuli vya jioni vinashuka, tuna furaha mno kuwa na mahali pa kuja. Wakati ulimwengu umechanganyikiwa mno nao haujui ambapo wanasimamia, tunafurahi kwamba Jina la Bwana ni Ngome Imara, na wenye haki huikimbilia, wakawa salama. Si kwa maneno mengi sana, bali, bali *ufunuo*.

Kwa hiyo, twaomba Baba, wakati nuru za jioni zingekuja wakati wa jua kuchwa, nasi twaamini kwamba huo ndio wakati tunaoishi—katika machweo ya jua. Basi kwa heshima sana tunakushukuru Wewe, Bwana, kutoka kwenye kilindi cha mioyo yetu, kwa ajili ya mambo ambayo Wewe umetutendea. Basi Bwana, kote katika nyakati zilizopita ninakushukuru Wewe kwa kuachilia maono yale ambayo Wewe umetoa—kila moja ya hayo kwa usahihi sana, na kila tafsiri ya ndoto imekuwa sawa kabisa. Kwa hiyo twajua ingeweza tu kuwa Wewe, Bwana, kwani sisi hupatikana na mauti—wote tumezaliwa katika dhambi, na hakuna kitu chema ndani yetu. Lakini kufikiria kwamba Wewe ungeweza kuchukua kitu kama binadamu na kumsafisha kwa Maji ya Neno na kwa Damu ya Kristo, na kunyoosha Mkono Huo kwa namna ambayo hata mtu hatumii mafikara yake, lakini kuruhusu Nia ya Kristo Ambaye ajua mambo yote. Ukairuhusu iingie ndani na kunena, na kutumia maskani. Asante, Baba. Sasa twalibariki Jina Lako Takatifu. Nasi twabariki kundi hili dogo usiku wa leo katika Jina Lako. Twambariki mchungaji, Ndugu Neville, mtumishi hodari wa Mungu. Twawabariki mashemasi,

wadhamini, na kila mshirika wa Mwili wa Kristo hapa na ulimwenguni kote katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

Na Loo, tunapoona hiki kivuli cheusi, chenye giza na cha kutisha kikiangukia uso wa Ukristo, twajua wakati unakaribia. Kutakuwa na Kunyakuliwa na Kanisa litatwaliwa. Bwana, tujalie tupige hatua taratibu, tukimtazama Mwazilishi na Mwenye Kutimiza, Kristo. Tukirimie hilo, Bwana, na tusogeapo mbele, sasa, katika Jina la Bwana Yesu kushughulikia mambo haya ambayo yamewekwa mioyoni mwetu, twaomba kwamba utakuwa pamoja nasi na utusaidie na ujipatie utukufu katika hilo, Bwana, kwani twajitoa Kwako, na Neno Lako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, kama una penseli na karatasi, ningewatakeni muandike mambo fulani au cho chote unachotaka kuandika; iweke tayari tu. Na halafu kwenye kanda, pia. Kama ukitaka kuandika Maandiko wakati wo wote, kwa maana naamini Maandiko ndiyo muhimu.

Sasa, twataka kusoma kifungu cha maneno usiku wa leo, au kusoma somo la Maandiko, kutoka katika Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo. Nami naamini kwamba huu ni Ufunuo wa Yesu Kristo kama ulivyoandikwa katika Kitabu. Na ufunuo wo wote mwingine usiokubaliana na ufunuo *huu* ungekuwa si sahihi. Naamini hilo lingestahili kunukuliwa tena. Ufunuo wo wote ambao hautapatana na Ufunuo huu na kuuleta Ufunuo huu kwenye Nuru, ni ufunuo wa uongo. Lazima uwe wa Kimaandiko.

Sasa, katika sura ya 10 ya Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo, nataka kusoma aya chache za mwanzoni, aya saba za mwanzoni—moja hadi saba. Basi sikilizeni kwa makini sasa, na mniombee.

> *Kisha nikaona malaika mwingine mwenye nguvu—mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, amevikwa wingu; na upinde wa mvua juu ya kichwa chake; na uso wake ulikuwa kama jua, na miguu yake kama nguzo za moto.*
>
> *Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa. Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi.*
>
> *Naye akalia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo. Na alipolia, zile ngurumo saba zikatoa sauti zao.*
>
> *Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao, nalikuwa tayari kuandika. Nami nalisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo ngurumo saba, usiyaandike.*
>
> *Na yule malaika niliyemwona, akisimama juu ya bahari na juu ya nchi, akainua mikono yake kuelekea mbinguni,*

> *Akaapa kwa yeye aliye hai hata milele na milele, yeye aliyeziumba mbingu na vitu vyote vilivyomo, na nchi na vitu vilivyomo, na bahari na vitu vilivyomo, ya kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya.*
>
> *Isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baragumu; hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii.*

Basi somo langu (kama ningeliita hivyo) usiku wa leo ni: *Hii Ndiyo Ishara ya Mwisho, Bwana?*

Sote twajua kwamba tunaishi katika wakati mzuri mno kwa Kanisa, lakini wakati wa kutisha mno kwa asiyeamini. Nasi twaishi katika mmoja wa nyakati za hatari zaidi ya zote—zote ambazo ziliwahi kuweko tangu ulimwengu uanze. Hakuna nabii, hakuna mtume, kamwe katika wakati wo wote, aliyewahi kuishi katika wakati kama huu tunaoishi sasa. Huu ndio wa mwisho.

Imeandikwa mbinguni. Imeandikwa juu ya uso wa dunia. Huandikwa katika kila gazeti. Huu ndio wa mwisho—kama unaweza kusoma maandishi. Manabii waliishi katika wakati ambapo maandishi yalikuwa ukutani kwa ajili ya taifa, lakini tuanishi wakati maandishi yamo ukutani kwa ajili ya wakati. Mataifa yote, dunia, kila kitu—wakati umefikia mwisho. Kwa hiyo yatupasa kuyachunguza Maandiko kuona saa ambayo tunaishi.

Siku zote, nabii wa kweli wa Mungu ataenda kwenye Maandiko. Kwa hiyo anafahamu yakini kwamba itakuwa hivyo. Katika Agano la Kale wakati manabii waliponena cho chote, daima alikuwepo mahali fulani nabii aliyekuwa na Neno—aliyedumu na Neno. Alimwangalia Mungu apate maono. Na iwapo ono lake lilihitilafiana na Neno; basi ono lake halikuwa sahihi. Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kulipeleka Neno Lake kwa watu Wake. Je! mnasikia vizuri huko nyuma?

Nashindwa nianzie wapi. Sasa, imekuwa heshima kubwa kwangu kujua kwamba maskani hii ilikuwa kanisa langu la kwanza. Ni jambo tukufu mno, na sitasahau kamwe ingawa mimi . . . Yesu akikawia nami ningeishi kuwa na umri wa mamia ya miaka, nitakumbuka siku ile niliyoweka jiwe la pembeni, hapo kwenye kona, na ono Yeye alilonipa asubuhi ile, la maskani hii. Na ninyi nyote mnakumbuka. Limeandikwa vitabuni, nalo limetimia kabisa. Hakuna hata chembe isiyotimia.

Na sasa, siamini kwamba kuna jambo lo lote Yeye alilonena, katika miaka hii yote ya maisha yangu, ambalo nimewaamibia watu, isipokuwa lile lililotokea. Na watu wengi wamekuja na ndoto ambazo Yeye ameniruhusu, kwa neema Yake, kuzifasiria watu. Na wengi wamekuja na ndoto na matatizo ambayo sikuweza kuyafasiri.

Lakini sikujaribu kuwaleteeni enyi watu ujanja, ambao una majibu yote. Nimejaribu kuwa mwaminifu na kuwaambia yaliyo kweli, nami ningewaambia tu, kama Yeye alivyoniambia. Kisha basi iliponijia, basi niliweza kuwaambia.

Nami nataka kuwaonya. Katika siku hii tunayoishi, kuna wengi. . .siyo. . .siyo kunena kitu cho chote kuwapinga watu, lakini unapoona mtu mwenye jibu kwa kila kitu, hilo linahitilafiana na Neno.

Yesu alisema, "Huko nyuma palikuwa na wenye ukoma zamani za Eliya, lakini ni mmoja tu aliyeponywa." Wajane wengi zamani za Elisha, lakini alipelekwa tu kwa mmoja. Basi tunaona kwamba kuna mambo mengi ambayo Mungu hufanya, na ambayo hawafunulii watumishi Wake, na hakuna mtumishi aliye mkuu kuliko Bwana wake. Halafu basi, Mungu hatashiriki utukufu Wake na mtu ye yote. Yeye ni Mungu. Basi wakati mtumishi anafikia mahali ambapo anajaribu kuchukua mahali pa Mungu, basi Mungu humuondolea uhai wake na kumpeleka mahali fulani, au kitu fulani. Yatupasa tukumbuke hilo.

Sasa, katika maono yale na tafsiri. . .Siwezi kukuambia tafsiri ya ndoto mpaka nione dhahiri, katika ono, ndoto ile ilikuwa nini. Na wengi wenu mnajua kwamba mmenisimulia ndoto zenu na hata hamngeielezea yote. Na nilipoiona ndoto ile, ikinirudia, niligeuka na kukwambia kwamba kuna mengi yake uliyoacha, na kisha kukuambia uliyoacha. Mwajua hii ni kweli. Iwapo ni kweli semeni, "Amina." Mnaona, mambo ambayo hamkuniambia. Kwa hiyo mnaona, ni kama Nebukadreza alivyosema, "Kama hamwezi kuniambia nilichoota, basi ningejuaje mnayo tafsiri yake?"

Lakini hizi dhana zote, haitupasi kuzichukua na kusema, "BWANA ASEMA HIVI." Haitupasi kufanya hivyo. Yatupasa kusikia sauti ya moja kwa moja (jibu toka kwa Mungu) kabla ya sisi kuweza kusema ni Mungu. Si dhana. Si mwamsho. Haidhuru inapigapiga kiasi gani, waweza ukaseme, "Naamini ingeweza kuwa namna hii," lakini unaponena, "BWANA ASEMA HIVI." Si wewe. Angalia jukwaani. Ulipata kuiona ikishindwa? BWANA ASEMA HIVI ni kamilifu. Haijashindwa kamwe. Na maadamu ni, BWANA ASEMA HIVI, haiwezi ikashindwa.

Lakini mpaka sasa Yeye amenilinda, kwa sababu nimemngojea. Sikujaribu kutafuta kupendwa na watu, au majivuno ya binadamu. Nimejaribu kuishi kwa unyenyekevu, na kuishi maisha ambayo nafikiri Mkristo anapaswa kuishi. Nami sikuweza kutenda hilo kwa uwezo wangu, lakini Yeye amelitenda, hadi siku hii. Kama ninavyosema, kwamba Yeye Ndiye ameniongoza.

Mambo mengi yangeweza kunenwa jinsi hii, lakini itachukua muda mrefu sana. Lakini ninyi nyote mnajua mambo haya, na sababu pekee nimewaambia mseme, "Amina," muda

mfupi uliopita—ninyi watu, ambao mmenisimulia ndoto, ndipo ningekuja kuwaambia mliyoacha—kwa sababu ujumbe huu unarekodiwa—watu wa mataifa yote watasikia haya, nao wanaposikia hiyo "Amina," basi watajua kwamba kuna sauti hapo ambazo ziko chini ya huduma hii, ambazo zinajua vema kuliko kutenda jambo lo lote baya, au kusema "Amina" kwa jambo ambalo si sahihi. Amina ni, na iwe hivyo. Ni kuidhinisha jambo.

Sasa, maishani mwangu mwote, tangu nimekuwa mvulana mdogo, kumekuwa na jambo ambalo limenihangaisha. Nami nimekuwa na maisha ya ajabu sana, vigumu kuyaelewa. Hata mke wangu hukuna kichwa chake na kusema, "Bill, siamini mtu ye yote angeweza kukuelewa."

Nikasema, "Mimi mwenyewe sijielewi," kwa sababu nilijitoa kwa Kristo miaka mingi iliyopita. Yeye ndiye aongozaye. Sijaribu kuyaelewa. Huenda tu Yeye aongozako, kadiri nijuavyo.

Ninashukuru sana kwa mke mzuri sana na watoto—na kwa mke wangu na watoto ambao wana imani kwamba nisingewaambia kitu cho chote kusicho sahihi. Hilo wanaamini. Kila wakati unapowaambia jambo lo lote, wao hulishikilia. Wanajua sitawaambia jambo lo lote lisilo sahihi. Nami hivi ningemwambia mmoja wa wana wa Mungu lisilo sahihi, basi? Siyo kwa makusudi, la bwana. Mungu anataka watoto Wake wapate mafunzo yaliyo sahihi. Nawe uwe mwaminifu kwao na mkweli kwao, Naye atabariki hilo, naamini.

Sasa, wakati wote katika safari, kumekuwa na mambo ambayo yametokea ambayo sikuyaelewa, na mojawapo ya mambo ambayo sikuyaelewa ilikuwa nilipokuwa kijana mdogo na maono hayo yangenijia. Ningeyaona na kuwaambia wazazi wangu mambo ambayo yangetukia. Walifikiri nilikuwa nimeshikwa na fadhaa tu. Lakini jambo la ajabu, ilitukia jinsi Hilo lilivyosema. Unasema, "Hilo lilikuwa kabla ya kuongoka kwako?"

Ndiyo. "Vipawa na miito havina majuto," Biblia ilisema. Umezaliwa humu ulimwenguni kwa kusudi fulani. Nawe hu . . . Toba yako haileti vipawa—vimekusudiwa awali kwako.

Sasa, na humo njiani—na nilipokuwa mvulana mdogo hamu yangu ilikuwa—sikuridhika katika nchi niliyoishi. Nilitamani, kwa namna fulani, kwenda magharibi.

Nami nilifanyiwa upasuaji, nilipopigwa risasi, nilipokuwa mvulana mdogo. Ndipo nilipopata jirudia kwa nusukaputi ya kwanza, nilifikiria nilikuwa kuzimuni—nikitumbukia chini. Ile nusukaputi ilinitoa fahamu. Nilipoteza fahamu kwa masaa manane, nafikiri. Walikuwa na wasiwasi juu ya kunifanya nipate kujirudia tena. Walinifanyia upasuaji mkubwa bila ya penicilini—damu. Miguu yote miwili karibuni ing'olewe

kwa bunduki ya marisaa—rafiki mdogo wa kiume aliachia bundukuki yake kufyatuka.

Kisha miezi saba baadaye, nilipata nusupakuti nyingine, na nilipozinduka kutoka katika dawa hiyo, nilifikiri nilikuwa ninasimama kule katika mbuga pana ya magharibi, na msalaba mkubwa wa dhahabu angani, nao Utukufu wa Mungu unaangaza kutoka kwake, na mimi nimesimama hapo hivi.

Hapo ile Nuru, ambayo mnaiona katika picha usiku wa leo, ambayo imehakikishwa kuwa Kiumbe cha Kimbinguni na uchunguzi wa kisayansi . . . Kwangu mimi ni Nuru ile ile ambayo ilimpiga Mt. Paulo. Ilikuwa Nuru ile ile iliyowaongoza wana wa Israeli, usiku. Umewahi kuangalia, hapa, Malaika huyu, Yeye alivikwa wingu. Unaona, mchana Yeye alikuwa wingu.

Sasa, Nuru ile ile—juu ya watu kutokuelewa, kwanza walifikiri kwamba ilikuwa makosa—kwamba nilikuwa ninajisemea tu hilo. Lakini ilitokea Roho Mtakatifu ana vyombo vya kisayansi, na watu hapo, kwa udhihirisho, nao wakachukua picha Yake mara nyingi. Nilisema, "Naona mtu aliyefunikwa na kivuli cha mauti"—kivuli cheusi juu yao.

Wiki chache zilizopita nilipokuwa mjini, na tunapohubiri . . . Hupaswi kuchukua picha, unajua, wakati wanahubiri, na wakati . . . (Ilikuwa vivyo hivyo hiyo ilipopigwa.) Lakini mtu fulani alikuwa na kamera. Nami nilimwambia bibi fulani aliyekuwa ameketi pale, mgeni. (Nilikuwa huko Southern Pines). Nikasema, "Kuna kivuli juu ya huyu Bi fulani (bibi ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu.) Ndio tu utoke kwa daktari na kansa mbili, moja kwenye kila titi, nawe umeishakatiwa tamaa. Umefunikwa na shela nyeusi ya mauti."

Na kitu fulani kikamwambia dada aliyeketi hapo karibu na ana kamera ya umeme, kikasema, "Piga picha." Naye hakutaka kufanya hilo. Hata hivyo, "Piga picha," na bado alikataa. Na kisha tena ikaja. Naye akanyakua ile kamera na kupiga picha, nayo iko hapo, kisayansi. Iko katika ubao wa matangazo. Kivuli cha shela nyeusi.

Halafu, wakati mwanamke huyu alipoamini na akaombewa, picha ilipigwa mara baadaye—safi. Nikasema, "Kile kivuli kimeishaondoka." Bibi huyo yu hai kwa neema ya Mungu.

Unaona ambalo ninamaanisha? Kama utasema ukweli—waweza uchekwe kwa muda kidogo, unaweza ueleweke vibaya kwa muda kidogo, lakini Mungu atalithibitisha hilo, kwamba ni kweli, kama utadumu tu nalo. Shikilia tu. Yaweza ichukue miaka kadhaa, kama katika Ibrahimu na wengineo, lakini Yeye sikuzote atalifanya liwe kweli.

Wakati malaika yule pale . . . na nafikiri, mbali na mke wangu, wapo watu hapa usiku wa leo tangu miaka thelathini iliyopita ambao walikuwa wamesimama karibu huyo

aliposhuka . . . Kuna mtu ye yote katika kusanyiko sasa ambaye alikuwepo pale wakati Malaika wa Bwana, ambaye alishuka chini mtoni mara ya kwanza, mbele ya watu, inueni mikono yenu. Ndiyo, hao hapo, unaona. Sasa naona Bibi Wilson aliinua mkono wake. Alikuwa amesimama hapo. Mke wangu pale—alikuwepo. Sijui ni akina nani kati ya hao wengine ambao walikuwa wamesimama ukingoni hapa, mbele ya watu wengi, wengi sana, nilipokuwa ninabatiza saa nane adhuhuri, na moja kwa moja toka kwenye mbingu za shaba, ambapo haikunyesha mvua kwa juma zima, huyu hapa akija kwa ngurumo. Akasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, wewe umetumwa na ujumbe wa kutangulia kuja mara ya pili kwa Kristo."

Umati mkuu kutoka wafanya biashara wa mji walikuwa wamesimama ukingoni na kuniuliza maana yake. Nikasema, "Hilo halikuwa kwa ajili yangu, ni kwa ajili yenu," akapanda juu akielekea nyuma huko upande wa magharibi. Alitoka moja kwa moja, akapaa juu kupita kilele cha daraja, akaenda upande wa magharibi.

Baadaye nilikutana na mtu mwenye elimu ya nyota, ambaye ni Mamajusi. Nao waliniambia kuhusu kundi la nyota ambazo zilikusanyika pamoja kwenye jamii kubwa ya nyota, wakati wale mamajusi wa Babeli walipoona kule kuelekea upande wa Palestina nyota hizi tatu katika kundi —mmenisikia mimi mara nyingi nikilisimulia. Unajua kwamba hilo limethibitishwa hizi juma chache zilizokwisha kwamba ni kweli?

Ndugu Sothmann, una lile gazeti usiku huu, po pote ulipo? Ipo gazetini—ukurasa wa gazeti la Jumapili, Desemba 9. Kwamba mwandishi wa habari aliendа kule na wakachimbua mambo yote haya na kwa kweli hivi sasa tunaishi . . . imethibitishwa, kwamba mwaka huu ujao ni 1970. Tumechelewa miaka saba kulingana na mawe yaliyochimbuliwa, na kuhakikishwa kwamba si sahihi. Imechelewa kuliko unavyodhania.

Sikumuona Ndugu Fred, sijui kwa nini. Ndugu Sothman, uko hapa? Unalo lile gazeti hapo, Ndugu Sothmann? (Yeye analo hilo gazeti.) Labda kesho usiku nitakuacha ulisome. Hatuna muda usiku wa leo.

Kwa hiyo, waweza kuona na kuangalia, sawasawa kabisa. Hao Mamajusi, Mamajusi wa Kiyahudi, huko Babeli, wakijifunza nyota, waliona nyota zile zikiingia katika kundi lao, na zilipofanya hivyo, walijua kwamba Masihi alikuwa duniani. Nao hapa wakaingia Yerusalemu wakiimba, (safari ya miaka miwili) "Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?" Huku na huko mitaani walikwenda, na mbona, Israeli waliwacheka. Kundi hili la wakithiri dini. Hawakujua cho chote kamwe kuhusu hilo. Lakini Masihi alikuwa duniani.

Na sasa. . .mnajua sehemu iliyosalia—kile walichosema. Sasa, tutalisoma hilo kesho usiku.

Sasa, tukija kwenye hili—kwamba maono hayakosei, kwa sababu yanatoka kwa Mungu. Na safarini mwote kumekuwa na jambo fulani linalonivuta, linalonivuta kwa nguvu. Basi, wakati Mamajusi waliponiambia mambo haya nilipokuwa mvulana tu—mlinzi wa wanyama. . .(au kabla ya hilo, naamini ilikuwa hivyo) kuhusu mambo haya, iliniogofya, kwa sababu niliogopa walichokuwa Mamajusi. Lakini baadaye niliona kwamba wale Mamajusi wa Biblia walikuwa sahihi, kwa sababu Mungu hulitangaza Mbinguni kabla ya Yeye kulitangaza duniani—kuchunguza sayari hizo za mbinguni.

"Mungu hana upendeleo wa watu wa mataifa yote," alisema Petro. "Sasa wale wanaomcha Yeye, katika mataifa yote Mungu huwakubali."

Na tunaona basi. . .Nilijaribu kusahau wazo lile lakini. . . Loo ingechukua masaa kadhaa kueleweka, jinsi mara zote—ilisogea namna hiyo, ikasogea namna hiyo, lakini niliogopa hilo. Huyu Mamajusi akaniambia, "Hutafanikiwa kamwe Mashariki." Akasema, "Ulizaliwa chini ya ishara fulani." Kisha akasema, "Wewe, ishara hiyo, hilo kundi la nyota, zilipopitana mle ndani, siku ya kuzaliwa kwako, zilikuwa zinaning'inia kuelekea magharibi, nawe yakubidi uende magharibi."

Nikasema, "Sahau." Sikujihusisha nalo kamwe. Hata hivyo daima, hiyo haikuliondoa moyoni mwangu.

Kisha, nilipokuwa hapo usiku ule kuhusu maono haya, sikuweza kuelewa. Ndugu zangu wa Kibatisti waliniambia jambo hilo ni la ibilisi. Ndipo basi wakati Malaika yule alipotokea, Yeye akaliweka vizuri kabisa katika Maandiko na akasema kama ilivyokuwa wakati huo, wakati makuhani walikuwa wakibishana kuhusu mambo—bila kujua wavae makoti gani, nguo, na kila kitu, na kubishana kuhusu tofauti zao —Mamajusi walikuwa wanafuata nyota ile kwenda kwa Kristo.

Wakati wahubiri waliposema kwamba Yesu ni mlaghai, Beelzebuli, pepo aliinuka akasema, "Twajua Wewe u nani—Mtakatifu wa Mungu. Kwa nini unakuja kututesa kabla ya wakati?"

Wakati Paulo na Sila waliposhuka wakaja wakihubiri Injili, maskini mpiga ramli, akiketi njiani. . .basi wahubiri wa nchi ile wakasema, "Watu hawa ni walaghai. Wanayavuruga makanisa yetu, na kadhalika, wakiupindua ulimwengu juu chini kwa upotovu wao."

Lakini kulitukia nini? Maskini yule Mamajusi (maskini huyo mpiga ramli) akasema, "Hawa ni watu wa Mungu wanaotuambia njia ya uzima."

Naye Paulo akaikemea roho ile ndani yake. Hakuhitaji msaada wo wote kushuhudia yeye ni nani. Yesu wakati wote aliwaambia wanyamaze. Lakini inaonyesha kwamba wakati mwingine pepo hujua mengi kuhusu mambo ya Mungu kuliko wajuavyo wahubiri. Walikuwa wameshikwa mno na dini. Ndivyo ilivyokuwa katika Biblia, na Mungu habadiliki.

Siku moja, nikishuka miaka mitano iliyopita toka kwa Ndugu Norman, nilikuwa naendesha gari barabarani. Ndio tu nilikuwa na mkutano juu kule, ndipo Bwana Mungu alinitokea katika ono. Nami nilikuwa nimeketi mbele ya lango langu, juu hapa nyumbani kwangu. Na ilionekana kuwa hali mbaya ya hewa.

Wengi wenu ninyi watu mtakumbuka ono lile. Limeandikwa katika kitabu changu cha maono. Niliyaandika kusudi niwe na hakika kwamba siyasahau.

Na katika ono hili nililoona, kulikuwa na kitu ambacho kimekuja kupitia kwenye njia, na kulikuwa na mawe yamezagaa pote uwani mwangu. Na kulikuwa na greda na mashine za kuparuzia ardhi huku na huko njiani, na miti ilikuwa imekatwa na kung'olewa. Nami nikaanza kuingia langoni, na lilikuwa lote limezibwa na mawe. Nami nikatoka niende kumwambia yule mtu, "Mbona hivi?" naye akawa mkali sana. Kanisukumia nyuma na kusema, "Hivyo ndivyo mlivyo ninyi wahubiri."

Nikasema, "Ninakuuliza tu, kwa nini unafanya hivi? Wewe unavuka upande wangu wa barabara, hapa. Kwa nini umefanya hivi?" Na yeye nusura anipige kofi, na akanisukumia nyuma.

Nami nikafikiria, "Nitamwambia tu kwamba hajui anachokizungumzia," na sauti ikanena ikasema, "Usifanye hivyo. Wewe ni mhubiri."

Nami nikasema, "Vema."

Kisha nikageuka, na upande wangu wa kulia, likiketi mbele ya lango, palikuwa gari la kukokotewa mbugani. Wajua nini—gari lililofunikwa, na farasi wamefungiwa kwake. Na mke wangu ameketi kukabili upande wa dereva. Kisha nikaangalia nyuma, na watoto wangu walikuwa wameketi nyuma kule. Nikapanda juu ya lile gari. Nikamwambia mke wangu, "Mpenzi, nimestahimili yote niwezayo kustahimili."

Basi nikakamata kamba, nikamvuta farasi aliyeongoza, kisha nikashika hatamu kuelekea magharibi. Basi sauti ikaniambia, "Jambo hili likitukia, basi nenda magharibi."

Ndugu Woods, ambaye ni kondrakta hapa kanisani mwetu, na mdhamini. . .Ni wangapi sasa wanalikumbuka lile ono? Mnakumbuka nikiwaelezeni? Hakika. Limeandikwa katika karatasi. Basi nikamwambia Ndugu Wood. . .Alinunua toka kwa kanisa sehemu hii iliyopo katikati pale. Alikuwa anataka kujenga nyumba ya mawe hapo. Nikasema, "Usifanye hilo,

Ndugu Wood, kwa sababu hawangekupa fedha zako kwake." Penginepo labda . . . hilo lilikuwa miaka mingi iliyopita—miaka mitano iliyopita—nikasema, "Labda watapitisha daraja lile hapa, na hayo mawe yalikuwa labda orofa yangu ya chini iliyombolewa na mapito yangu na kadhalika vikiwa nje hapa. Badala ya kuwa mawe, ilikuwa ni vipande vikubwa vya saruji, na basi watayaweka hayo hapa chini; kwa sababu walisema katika gazeti hilo ndilo wanajaribu kufanya. Vema, hakuijenga. Hatimaye waliamua yapata mwaka mmoja baadaye, au miwili, wataipitishia upande huu. Kwa hiyo hilo likatosheleza mambo, kwa hiyo nililisahau tu, na kuliachilia.

Sasa, jambo la ajabu lilitokea mnamo mwaka mmoja uliopita. Nilikuwa na ibada usiku mmoja kwa Ndugu Junior Jackson, anayeketi papa hapa, mhubiri wa Kimethodisti ambaye amempokea Roho Mtakatifu, na amebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, na anahudumia moja ya makanisa mashirika yetu.

Kukuonyesha tu jinsi ambavyo Mungu hushughulika na watu hawa —nasema hili kwa moyo wangu wote —sijui kuhusu kusanyiko lo lote katika ulimwengu mzima, linalokusanyika kwa pamoja tena, ambapo naamini Roho wa Mungu yupo kuliko alivyo katika kusanyiko hili. Wana tofauti zao. Hakika hawapo ambapo wanapaswa kuwa, hakuna hata mmmoja wetu, lakini wapo karibu kama mtu mwingine ye yote nimjuaye.

Sasa kukuonyesha, nikijua ambalo lingetendeka, Ndugu Jackson aliota ndoto. Hangeweza kuisahau. Basi nilikuwa ninaliacha kanisa lake, na hakuweza tu kulivumilia jambo hilo.

Imekuwa muda gani Ndugu Jackson?

[Ndugu Jackson: "Niliipata ndoto ile mnamo Februari ya '61."—Mh.]

Februari ya '61 alipata hiyo ndoto. Basi akanijia, akasema, "Jambo fulani limo moyoni mwangu, yanibidi nikuambie, Ndugu Branham."

Nikasema, "Endelea, Ndugu Jackson."

Naye akasema, "Niliota ndoto," na hiyo hapo! Nikakaa tu kimya. Nikasikiliza na kuangalia. Akasema, "Niliota kwamba kulikuwa na kilima kikubwa sana, ilionekana kama nje katika shamba mlimokuweko majani ya samawati, au kitu fulani." Akasema, "Juu kwenye kilele cha kilima hiki, ambapo maji yameondoa udongo, palikuwa na jiwe la kileleni juu ya kilima; kama kilele cha mlima. Ilikuwa mwamba mtupu, hakuna nyasi. Na ambapo maji yalitiririkia, yalikuwa yameandika namna ya maandiko juu ya mawe haya, nawe ulikuwa umesimama pale ukifasiri maandiko haya katika mawe haya." Akasema, "Sisi sote . . . " (na maneno yake ndiyo haya:) "Ndugu kutoka Georgia, na kutoka kila upande, sote tulikuwa tumesimama pamoja,

tukikusikiliza ukifasiri hayo maandishi ya ajabu katika mawe yale . . . mlima ule."

Kisha akasema, "Ndipo ukaokota kitu fulani, kama kutoka hewani, kitu kama mtaimbo wa kuvunjia au mtaimbo," sivyo, ndugu? Kitu kama hicho—mtaimbo wa kuvunjia, mkali hasa, ndipo kasema kwamba "Jinsi ulivyolifanya jambo hilo, sijui." Ndipo akasema, "Uligonga kilele cha ule mlima, ukakikata, ukainua kifuniko chake. Kilikuwa katika umbo la piramidi. Nawe ukakikata na kuinua kifuniko chake." (Sasa hilo lilikuwa miezi na miezi na miezi kabla ya kuhubiriwa ujumbe wa piramidi.) Naye akasema, "Chini ya hilo palikuwa na jiwe jeupe, jiwe gumu sana, nawe ukasema, 'Jua, au nuru, haijawahi kuangaza juu ya hili hapo kabla. Angalieni hili. Tazameni hili'."

Na hilo ni kweli, kwa sababu katika kufanyizwa kwa ulimwengu, ulimwengu uliumbwa kabla ya kuwepo nuru. Sote twajua hilo. Mungu akatulia juu ya maji, halafu hapo mwanzo akatamka iwe nuru. Na kiasili, chini kule katika wakati wa huko kufanyizwa, nuru haikuwa imeangazia lile jiwe kamwe.

Naye akasema, "Angalieni hili. Nuru haijawahi kuliangazia hapo kabla." Basi wakati wote walipokaribia, niliwaambia waangalie hilo, na wote wakaja kuangalia mle ndani. Lakini alisema wakati walikuwa wakiangalia mle ndani, aliangalia kitongotongo (naamini ndivyo ilivyokuwa) na akaniangalia. Nikaondoka kisirisiri upande mmoja na nikaanza kwenda kuelekea magharibi; kuelekea machweo ya jua, nikakwea kilima, nikatelemka chini ya kilima, nikakwea kilima, nikatelemka chini ya kilima, huku ninazidi kuwa mdogo, kisha nikatoweka.

Akasema, basi nilipofanya hivyo . . . akasema, "Basi wandugu wakageuka, baada ya muda kidogo, na kusema, 'Ametoweka? Ameenda wapi?'" Ndipo akasema baadhi yao wakaenda huko, baadhi yao wakachukua njia moja, na wengine nyingine, lakini wachache sana walibakia na wakaendelea kuangalia kile ambacho niliwaambia.

Sasa angalia, tafsiri ya ndoto hiyo, ambayo sikumwambia hata kitu kimoja, au hakuna hata moja ya hizi nilimwambia ye yote wao. Lakini nilisema, "Ndiyo," na moyo wangu ukitetemeka. Nilikuwa ninaangalia. Sasa, yale maandishi ya siri . . . ngojeni nitayaacha tu kidogo.

Si muda mrefu uliopita Ndugu Beeler . . . Ndugu Beeler kwa kawaida huwa pamoja nasi. Uko hapa Ndugu Beeler? Ndiyo, nyuma huku. Billy alisema, "Ndugu Beeler amehangaika mno. Aliota ndoto ya ajabu." Nilikwenda kwa Ndugu Beeler, naye alisema (mle nyumbani mwake usiku mmoja wakati nilipoitwa kwa simu). Naye akasema, "Ndugu Branham, niliota ndoto ya ajabu. Kasema niliota kwamba nilikuwa nikifuata kijito cha maji kuelekea magharibi. Na kulikuwa na barabara upande wa

kushoto, nami nilikuwa upande wa kushoto, nikienda magharibi kwa hiyo njia, ilivyoelekea, nikiwatafuta ng'ombe. Na upande wa kulia (ilitokea niliona hayo baada ya kufika chini kule) ulikuwepo hapo. Nawe ulikuwa unakusanya kundi kubwa la ng'ombe, na kulikuwa na malisho mengi huko. Kisha akasema ukawachukua hao ng'ombe na ukaanza kuwaelekeza upande wa juu wa mto." Na ilivyoonekana (lazima nilimwashiria kwamba awaangalie wale ng'ombe) akasema, "Sasa itakuwa rahisi kwa hao ng'ombe, najua wataendea barabara ile yenye pingamizi chache sana, lakini Ndugu Branham anawataka wabakie upande wa kulia wa mto. Kwa hiyo nitapita barabara hii, na kuwazuia wasije wakavuka mto upande huu na kuwaweka upande ule," lakini aliona, sikuwafuata wale ng'ombe, lakini nilikwenda upande wa magharibi.

Akasema, "Hapana budi anawatafuta waliopotea."

Mara alipoisimulia tu ile ndoto, nikaiona. Na basi, angalia, alisema kwamba alinitazama kitongotongo kidogo, kwa hiyo akarudi ili aangalie. Naye akasema kwamba nilikuwa ninakuja kwenye mlima mkubwa sana, mara nikatoweka. Naye akashangaa imekuwaje. Akashuka, na kisha aliona kijito kidogo kando yake ambacho kiligawanyika upande wa kushoto (nafikiri hilo ni sahihi, Ndugu Beeler). Ndiyo. Naye aliona kando yangu kulikuwa na maporomoko ya kutisha. Ndipo basi, akafikiria huenda nimetumbukia katika maporomoko yale nikaangamia. Kisha akaona, naye alisema aliangalia huku na huko matokeo ya maporomoko hayo ambayo yaliangukia upande huu, nayo yalikuwa yakisababisha kisima cha chemchemi kububujika, lakini yale maji hayakuwa yakirudi ardhini. Akaangalia upande ule wa pili wa ule mkono wa mto, au kile kijito kidogo, naye akaona wanyama wadogo wenye masikio ya duara. Akasema, "Naamini nitamchukua mmoja." Naye akavuka.

Kisha akawa ananiwazia. Basi akapanda juu ya kilima kidogo kuangalia kule upande mwingine aone iwapo kuna mwamba mdogo na mwembamba nilikozungukia, lakini akasema, "Hapakuwa na cho chote." Naye alifadhaika, akasema, "Ni jambo gani limetukia kwa ndugu yetu? Nashangaa kitu gani kimempata Ndugu Branham?" Alipoogopa, akasema kwamba alinisikia nikinena. Nilikuwa nimesimama juu ya kilele cha mlima, na nikamwambia Ndugu Beeler tafsiri ya ndoto ambayo nilimpa si muda mrefu uliopita, nikamwambia amngojee Bwana, kwamba siku moja ningekutana naye kwenye kisiwa na alikuwa hapo.

Sasa, tafsiri ya ile ndoto ni hii. Kwa vile kile kijito kilikuwa kipana, kilikuwa Kijito cha Uzima. Nilikuwa nikienda upande wa magharibi juu yake, na vivyo hivyo yeye, kwa sababu alikuwa barabarani . . . alikuwa akikimbia katika barabara hii, na upande wa pili kulikuwa na nyasi nyingi, lakini vichaka vingi, miiba, na msitu. Lakini mle ndani mlikuweko na

nyasi nyingi. Basi hivyo ndivyo tunavyomtafuta Bwana, na chakula cha Bwana, kwa shida. Kukusanya wale ng'ombe—ilikuwa kanisa hili. Kuwaweka upande wa pili. Ng'ombe kwa kawaida hutembea kwenye barabara laini, madhehebu, kama wanaweza—ambapo barabara iliwakilisha madhehebu.

Nilimwelekeza upande wa juu wa barabara kuhakikisha kwamba hawakwenda kwenye madhehebu yo yote. Kwa vile aliona ukuta, ambao haupenyeki, ambao ulinizuia kwenda magharibi—ilikuwa ni ile kesi ya kodi ya serikali. Hakuna anayeweza kufahamu jinsi nilivyotoka katika hiyo. Ilikuwa ukuta ambao ulinizuia, lakini Bwana alinipitisha katika hilo, na nikaimaliza. Nami nitakutana nawe, Ndugu Beeler, kwenye kisiwa.

Kwa hiyo, sasa basi mara baada ya hilo, Ndugu Roy Roberson. . .Ndugu Roy, upo hapa usiku wa leo? Ndiyo, naamini . . .Ndiyo, kule upande ule. Alinipigia simu, naye aliota ndoto. Aliota kwamba tulikuwa tunakusanya ngo'mbe. (Sasa hiyo ni ya tatu.) Kuwakusanya ng'ombe. Nyasi zilifika tumboni—chakula kingi sana. Sisi sote ndugu tulikuwa pamoja. Basi tulikuja mahali fulani tupate kula chakula cha mchana, ndipo Ndugu Fred Sothmann akainuka na kusema, "Eliya, yule nabii mkuu, atazungumza kutoka hapa leo adhuhuri." Ndipo sote tulipomaliza chakula, kila mtu alienda zake, naye alishangaa kwa nini hawakungojea kusikiliza hilo likinenwa.

Sasa, waona jinsi hiyo inavyolingana na ya Ndugu Jackson? Unaona hiyo sawasawa, inagonga sawasawa na alivyosema Ndugu Beeler? Hakuna aliyengojea apate kufahamu.

Angalia, mara baada ya hilo, Dada Collins. . .Upo hapa, Dada Collins? Aliota ndoto ya kuwepo hapa kanisani, na kulikuwa na arusi iliyokuwa karibu kufanyika. Na alipotenda hivyo, alimuona bwana arusi akija katika ukamilifu, lakini bibi-arusi hakuwa mkamilifu sana, hata hivyo alikuwa ni Bibi-arusi. Sasa, hilo ni Kanisa. Kulikuwa na kitu kama meza ya Bwana, au ibada fulani, ikiendelea hapa—kama chakula cha jioni kikiandaliwa. Na kwa namna fulani kilimshangaza mno kwa sababu Ndugu Neville alikuwa akihudumu chakula cha jioni kanisani, lakini akasema kilikuwa chakula kizuri sana alichowahi kuona. Yeye alikuwa na njaa sana. Akafikiri labda, katika ile ndoto kwamba asingekihudumu, na yeye na Ndugu Willard walikuwa wanaenda kwenye Nyumba ya Ranchi wakale. Na walipoondoka, taa kwenye upande wa kulia ikazima. Sasa mnajua hilo lina maana gani.

Sasa, kile chakula—Bibi-arusi si mkamilifu, lakini Bwana Arusi ni mkamilifu. Bibi-arusi hajawa mkamilifu bado, lakini kile chakula ambacho kilikuwa kinatolewa hakikuwa chakula halisi, ni chakula cha Kiroho ambacho mmekuwa mnakula

wakati wote. Hebu nikomee hapa kwenye ile ndoto ya nne, muda kidogo tu.

Mnakumbuka Ndugu Fred Sothmann, Ndugu Banks Wood, tulipokuwa huko Arizona mwaka uliopita, tulipokuwa nje tukiwinda nguruwe wa mwitu, na Bwana akanena. Hamjui mambo aliyoyafanya Yeye kikamilifu, akionyesha ambacho kingetukia, tulipokuwa tukitembea barabarani. Kama hilo ni kweli, ninyi ndugu wawili semeni, "Amina." Hakosei kamwe.

Kisha nikaona katika ono tulipokuwa tukiendesha gari siku moja, ono la Bwana lilinijia, nami nilikuwa ninajitayarisha wakati ule, niliporudi nyumbani, kwenda ng'ambo. Na nilipokwenda ng'ambo, vyema, niliona melini . . . au kando ya bahari, ambapo meli zilitokea. Napo palikuwapo na mtu mmoja mfupi, naye alisema, "Nimekuandalia mashua, Ndugu Branham." Na ilikuwa kijimtumbwi kidogo sana, yapata urefu wa futi moja, ila kilikuwa cheupe kama theluji. Kisha akaniambia, "Huu ndio utakaovukia."

"Loo," Nikasema, "Haunitoshi."

Akasema, "Utasafiri maili arobaini kwa saa huku na huko namna hii." (Yaani huku na huko ukingoni.)

"Lakini," nilisema, "hautanivusha." Ndipo basi aliangalia chini, akasema, "Enenda kama wanavyoenenda." Kisha nikaangalia, na walikuwepo Ndugu Fred Sothmann na Ndugu Banks Wood wameketi katika mtubwi uliopakawa rangi ya kijani, na turubai za kufanya kambi nyuma yake —Ndugu Bank akiwa na kofia iliyobinuliwa hivi, Ndugu Fred akiwa na yake imefinywa mdomoni. Akasema, "Enenda kama wao."

Nikasema, "La, sitaenda." Kisha mtu huyu akawaambia (mtu yule mdogo) akasema, "Ninyi ni mabaharia?"

Ndugu Banks akasema, "Ndiyo."

Ndugu Fred akasema, "Ndiyo."

Lakini nikasema, "Hao si mabaharia. Mimi ni baharia, na najua nisingeenda kwa huo, na nina hakika nisingeenda hivyo."

Akasema, "Kwa nini usiende pamoja nao?" Nikasema, "La, la."

Vyema, nikageuka, nilipogeuka, ikawa kwamba mtu yule mdogo bandarini alitokea kuwa, ndugu yangu mzuri, Ndugu Arganbright.

Nami nilirudi katika ono hili, na palikuwa na jengo dogo refu, kisha sauti ikaniambia, (na ninyi nyote mnakumbuka hili, au wengi wenu) sauti ikaniambia, "Lete chakula. Kihifadhi mle ndani. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuwaweka hapa, ni kuwapa chakula." Nami nalileta . . . nilikuwa nimeleta mapipa makubwa yamejaa karoti nzuri sana na mboga nzuri na mambo kemkemu niliyoona. (Mnakumbuka, sasa, lile ono?) Sasa . . .

Na niliwaambia baadaye tafsiri ile ilikuwa nini. Nilitakiwa niende Zurich, Switzerland, pamoja na Ndugu Arganbright kwa mkutano wa siku tano. Niliwaambia ndugu kabla haijatokea, "Sitakwenda."

Basi nalikuwa kule chini na Ndugu Welch Evans, chini huko, wakati nilipotoa tafsiri hiyo.

Usiku mmoja, naamini Ndugu Welch alikuja akanichukua, (tulikuwa tunaenda kuvua samaki) na akasema Ndugu Arganbright alikuwa ananiita. Nikasema, "Sawa, hivi ndivyo ilivyo. Wanataka kunizuia kwenda." Na mara nyingi . . . (siyo kupitia Ndugu Miner—yeye ni mmojawapo wa marafiki wazuri sana) lakini wakati mwingine, kama wanaweza tu . . . kama wanafikiri wewe utahubiri jambo fulani ambalo linapinga mafundisho yao, wao hutangaza tu kwamba utakuwa pale kusudi marafiki wako wahudhurie. Basi walisema . . . Ndugu Arganbright alinipigia simu akasema, "Ndugu Branham," (vile tu Roho alisema) akasema, "njoo, na uje na mke wako, kwa sababu haitakubidi kuhubiri sana, kwa sababu nafikiri wamekuwekea tu usiku mmoja." Kisha akasema, "Huenda hata usihubiri huo usiku mmoja."

Ndipo nikasema, "La."

"Vema," ilisema, "Njoo, wewe na mke wako, ninyi nyote njoni, unaona, na kama mkija, nitawachukua mkaitalii nchi. Mke wangu na mke wako, na hao wote, tutaizuru Switzerland na kule Palestina."

Nikasema, "La."

Nilikuwa na ile tafsiri. Nilimwambia Ndugu Welch au Ndugu Fred na hao wengine, "Nitawaambia asubuhi, lakini yabidi kwanza mke wangu aseme kitu." Nami nilipompigia simu, basi alikataa kwenda. Nikasema, "Hii hapa." Unaona.

Sasa hiyo mashua ndogo nyeupe ilikuwa ni ule mkutano mmoja. Ni sawa kwenda po pote hapa, kwenye ukingo, na mkutano mmoja, lakini haitoshi (ingawa ulikuwa mweupe na mzuri) kuniita mimi kwenda ng'ambo.

Ndugu Fred na Ndugu pale (waliowakilishwa katika ono) waliwakilisha: nenda kama mtalii; kwa kujifurahisha. Lakini sikujali kufanya hilo. Na kuwakataa wao kuwa mabaharia—ilimaanisha hawakuwa wahubiri. Lakini mimi nilikuwa mhubiri. Halafu basi chakula kile katika lile jengo dogo refu—sikwenda ng'ambo; basi nilirudi kwenye jengo hili dogo, na tukanasa dazan za kanda za piramidi na kila kitu, kuwaonyesha watu saa tunayoishi.

Sasa linganisha hilo na zile nyingine, zile ndoto. Hili lilikuwa ono. Kile chakula; hiki hapa. Mahali penyewe ni hapa.

Angalia, basi kulitukia nini? Basi mara baada ya ono hilo la nne kuja, (au ndoto ya nne niliyoambiwa) akaja Ndugu

Parnell. Yupo hapa mahali fulani. Papa hapa. Naye Billy hakuwa hapa, na mtu huyo alikuwa ana bidii sana ya kujua. Anatoka Bloomington naamini au Bedford? Lafayette, akifanya mikutano. Basi aliota ndoto, kisha akaja kwa Ndugu Wood akasema, "Siwezi kabisa kujizuia. Sina budi kuisimulia. Yabidi nimwambie Ndugu Branham. Inanisumbua." Naye Mungu ajua, hapana ndoto moja kati yao. Zilikuja tu moja, mbili, tatu, nne, tano, sita.

Ndugu Parnell akasema, "Nilikuwa na ndoto ya ajabu. Niliota kwamba nilikuwa naenda kufanya mkutano juu kule, na kwa namna fulani kulikuwa na mkutano hapa katika kanisa lililoonekana kama jipya." Kisha akasema, Hili kanisa jipya, jinsi lilivyokuja, kwamba alishangaa kwa nini walikuwa hawashirikiani kati yao wawili, au kitu kama hicho. Basi akasema alikuwa amesimama hapa akafikiri, "Vema, nimekuwa ndani hapa, nitangojea tu, kisha nitahudhuria ibada." Akasema mtu akaja akipita katika jengo amevaa suti ya kahawia na kitabu—nafikiri alikuwa anaandika. Naye akamwambia Ndugu Parnell. . . Akasema, "Huu si mkutano wa kila mtu. Ni wa mashemasi tu na wadhamini." Vema, kwa namna fulani alijisikia ameudhiwa. Kwa hiyo alitoka nje ya lile kanisa jipya, kanisa lililojengwa, au hili linalotengenezwa—linalotengenezwa; naye alipotoka nje theluji ilikuwa inaanguka—hali mbaya ya hewa, majira ya kipupwe. Na hapana hata mmoja wa watu hawa aliyejua cho chote kuhusu hili.

Basi alipotoka nje, nilikuwa nimesimama pale, nikiangalia kuelekea magharibi. Basi nikasema, "Usiudhike, Ndugu Parnell. Nitakwambia utakalotenda."

Naye Ndugu Parnell na ye yote wa hao wengine wanajua kamwe sikuwapa tafsiri yo yote. Ni sasa hivi. Ingawa niliiona walipoisimulia. Uliona jinsi nilivyoondoka huko haraka, Ndugu Parnell, nisije nikakusimulia? Basi niliondoka nikaenda zangu na hata sikusema neno kwa Ndugu Woods au mtu ye yote yule. Hata mmoja. Niliiacha tu, kwa sababu nilitaka kuona inakoelekea. Je, mmenisikia nikisema hivi majuzi, "Nina wasiwasi"? Ndiyo hiyo.

Ndipo basi, Ndugu Parnell, alisema kwamba nimemwambia, "Ndugu Parnell, anza, na mahali pa kwanza utakapofika ni Zippora," linalomaanisha kistari, au kituo au kitu fulani. Nikasema, "Usikae hapo." Basi enenda pengine, na utamwona kizee mwanamke; basi usisimame pale. Nenda tena, utamwona mwanamke mkongwe—usisimame hapo. Na muda wote tulipokuwa tunazungumza, tulikuwa tunatembea katika theluji. Kisha nikasema, "Nenda mpaka umwone mke wangu, na utakapomwona mke wangu, simama hapo." Basi akasema aliangalia, nasi tulikuwa tumetoka kwenye theluji, katika jangwa. Na nilikwisha toweka. Naye akaangalia nyuma akamwona mke wake akichota maji kwenye kisima cha bomba,

na mhubiri fulani akimvuta, kumwondoa kwenye lile bomba. Mkewe alikuwa akimwangalia yeye—naye akaamka.

Hii hapa tafsiri ya ndoto yako: (Basi ningelikwambia usiku ule, lakini niliondoka tu.) Kwa kuwa huyo Zippora, na mwanamke mmoja kizee, na mwanamke mwingine mkongwe kupindukia—hayo ni makanisa. Unaona? Na Zippora, akiwa hasa mke wa Musa—Zippora— na tunaona kwamba nilimwambia asisimamie walipo hao, haidhuru ni wa kale jinsi gani, yalikuwa ni madhehebu. Usisimamie kwao! Wakati wao umekwisha. Lakini ajapo kwa mke wangu, ambalo ni Kanisa langu ambako Yesu Kristo amenipeleka mimi katika siku hizi za mwisho, nalo ndilo hili hapa! Simama hapo! Nami nilikuwa nimekwenda upande wa magharibi.

Halafu, Dada Steffy (anaweza asiwepo hapa kwa sababu amekuwa hospitalini) sijui . . . Dada Steffy . . . Ndiyo, huyu hapa. Dada Steffy alikuja nyumbani kwangu kwa maombi kabla ya kwenda hospitalini kupasuliwa, kwamba Mungu angemsaidia na kumbariki, na hakika Yeye alifanya hivyo.

Naye akasema, “Niliota ndoto ya ajabu, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Naam.”

Ndipo akasema, “Niliota kwamba nilikuwa huko magharibi kisha . . . ” (hiyo ni ya sita) naye akasema, “Niliota nilikuwa magharibi, nayo ni nchi iliyotandaa, nami nilipotazama, palikuwepo na mwanamume mzee sana mwenye ndevu ndefu nyeupe amesimama juu ya kilima, na nywele tu alizokuwa nazo, ziliningʼinia usoni mwake, naye alijizungushia kitu cheupe—kitu fulani—vazi, upepo ukilipeperusha.” (Nafikiri hilo ni kweli, Dada Steffy, hivyo.) Naye akasema, “Nilizidi kusogea karibu; alikuwa amesimama kwenye kilele cha mlima, akiangalia upande wa mashariki. Naye akasema, “Nilishangaa, ‘Mzee huyu ni nani?’” Naye akasogea karibu zaidi, karibu zaidi, na alipokaribia zaidi, akatambua alikuwa ni nani. Ilikuwa ni yule Eliya asiyekufa, yule nabii, akisimama pale akiangalia mashariki.

Akasema, “Sina budi nimuone!” (Alikuwa na haja:) Naye akakwea kile kilima mbio na kuanguka chini pale kuzungumza naye na katika jina la Eliya, akasema wakati alipozungumza, alisikia sauti ikisema, “Unataka nini, Dada Steffy?” Kumbe ni mimi.

Ndoto yako ilitimia pale pale, Dada Steffy. Kwa maana, mara baada ya hilo, nilikwenda Lousville. Ulichokuwa unahitaji ni yale maombi—kuona kwamba alifanikiwa hospitalini; na ile ishara ya mimi kwenda magharibi, nikiangalia mashariki, kwa ajili ya kundi langu.

Angalia, wakati . . . Nilikwenda Louisville, nami niliporudi, kwa namna fulani nilianza kuelekea langoni, na hapo

palikuwepo na vigingi vilivyopigiliwa upande wa pili wa lango langu. Bwana Goynes, anayeishi katika mtaa huu hapa, alikuwa anatembea njiani. Akasema "Billy, njoo hapa." Akasema, "Yakubidi uondoe malango yako na kadhalika—ua, kitalu cha mawe, na malango."

Nikasema, "Vema, sawa Bill." Nikasema, "Nitalifanya hilo. Lini?"

Akasema, "Nitakuambia. Nitakujulisha ni lini."

Nikasema, "Sawa, wataanza kazi mwakani."

Nikasema, "Sawa."

Kwa hiyo nilianza kurudi ndani ya nyumba, na mke akasema, "Yanibidi niende kununua vyakula haraka sana." Nikashuka nikaenda njiani, na mvulana, Raymond King, ambaye ni mhandisi wa mji —sikuzote nilimwita "Sikio la tope" kwa sababu tulipokuwa watoto wadogo tukiogelea pamoja, alimpiga jamaa mmoja kwenye sikio na donge la tope, na sikuzote tulimwita, "Sikio la tope." Anakaa hatua chache barabarani toka kwangu—yapata mlango wa pili chini ya Ndugu Woods.

Na kwa hiyo nikasema, "Tope, njoo hapa kidogo."

Akasema, "Sawa, Billy." (Akaja kule.)

Nikasema, "Kile kijiti ulichopigilia . . . "

Akasema, "Billy, watavichukua vyote— miti yote hii, vitalu hivi, kila kitu hakina budi kiondolewe."

Nikasema, "Vema, mhandisi aliniambia kwamba mali yangu iliingia katikati ya barabara."

Akasema, "Ndiyo, lakini wataipanua. Wataichukua kwa vyo vyote."

Akasema, "Yangu pia."

Nikasema, "Vema Ndugu Wood ni mwashi wa mawe," nikasema, "Nitamwita tu alisogeze nyuma."

Akasema, "Billy, usiiguse. Mwachie kondrakta afanye hilo. Huyo ndiye mwenye mamlaka, siyo?"

Nikasema, "Ndiyo bwana."

Akasema, "Mwache alifanye." Akasema, "Unajua ninalomaanisha."

Nikasema, "Ndiyo."

Nikageuka, mara nikakumbuka kitu fulani.

Nikaenda nyumbani, nikaingia chumba changu cha kusomea, nikachukua "kile kitabu," na ilikuwa pale. Haikuwa matofali ya saruji—ilikuwa ni mawe. Nikasema, "Meda, jitayarishe."

Ndoto sita dhahiri, kisha lile ono likazikamilisha. "Mambo haya yatakapotimia, shika njia uende magharibi."

Nikapiga simu Tucson. Ndugu Norman ana nyumba kule. Sijui niendako. Sijui la kufanya. Nipo tu katika... Nimesimama...Sijui la kufanya. Ninaacha makazi ambayo hainibidi kuilipia kodi. Mshahara wangu ni dola mia moja kwa juma. Karibuni yanibidi kulipa dola mia moja kwa mwezi kwa nyumba. Niko papa hapa na ndugu zangu na dada zangu ambapo ninapendwa. Nami naenda, sijui wapi. Sijui kwa nini. Siwezi kuwaambieni kwa nini. Lakini kuna jambo moja tu nijualo: kufuata tu yale Yeye aniagizayo kufanya. Sijui niende wapi. La kufanya, si juu yangu...

Nadhani Ibrahimu alijisikia namna hiyo wakati Yeye alipomwambia, "Vuka mto." Hakujua la kufanya. "Kuwa mgeni,"—ajitenga. Sikujua la kufanya.

Jumamosi iliyopita asubuhi, juma moja kutoka jana, mnamo kama saa tisa usiku, nilikuwa nimeamka nikanywa maji, nikamfunika Joseph katika chumba chake, na halafu nilikuwa nimerudi na kujilaza chini nikaingia usingizini. Nilipoingia usingizini...(sasa ninamalizia hizi ndoto ndogo na mambo mengine, ili muone msingi wa kile ninachotaka kusema) nilimfunika Joseph, kisha nikarudi, nikajilaza chini nikaingia usingizini; ndipo naliota ndoto: nami niliota kwamba niliona mtu aliyedhaniwa kuwa baba yangu, ingawa lilikuwa ni jitu kubwa mno; kisha nikaona mwanamke aliyedhaniwa kuwa mama yangu, ingawa hakufanana na mama yangu. Basi mtu huyu alikuwa bahili sana kwa mkewe. Alikuwa na fimbo ya pembe tatu, ambapo amepasua mti huu na kufanya—wajua unapopasua kuni kukingama gogo hutengeneza fimbo ya pembe tatu —na kila wakati mwanamke huyu angeanza kusimama, angemshika tu shingo, kampiga kichwani, na kumwangusha chini. Basi angelala pale, anadharau na kulia, na kisha angeanza kuinuka tena. Yeye angetembea huku na huko kwa fahari, kifua mbele—jitu kubwa mno— na wakati yule mwanamke angeinuka tena, angemkaba shingo, achukue fimbo hii ya pembe tatu, na kumpiga nayo kichwani—akamwangusha chini. Anarudi nyuma, kifua mbele kana kwamba ametenda tendo kubwa.

Nami nilikuwa nimesimama kando nikiangalia hili. Nami nikawaza, "Simwezi mtu yule. Ni mkubwa mno. Tena yeye anadhaniwa kuwa baba yangu. Lakini yeye si baba yangu." Nami nikasema, "Yeye hapaswi kumtendea mwanamke yule vile." Na kwa namna fulani akanihangaisha. Hivyo basi, mara moja nikapata ujasiri wa kutosha, nikamwendea, nikamkamata kwenye kala, nikamgeuza. Nami nikasema, "Huna haki ya kumpiga." Nami niliposema hilo, misuli ilikua—nilionekana kama jitu. Yule mtu akaangalia misuli ile, ndipo akaogopeshwa nami. Nikasema, "Hebu mpige tena, utapambana nami." Na kwa namna fulani akasita kumpiga tena. Ndipo nikaamka.

Nami nililala pale muda kidogo. Nikawaza, “Hilo ni nini? Ni ajabu ningeota kuhusu mwanamke yule.” Katika muda mfupi tu, Huyu hapa hapa anakuja. Nilikapata tafsiri.

Mwanamke yule anawakilisha kanisa la ulimwengu leo—ulimwengu wote. Nilizaliwa mumu humu katika mchafuko huu, nami nipo hapa. Anapaswa kuwa namna fulani ya mama wa . . . kama angekuwa mama wa makahaba—lakini hata hivyo nilizaliwa mumo humo. Na yule mume ni madhehebu ambayo yanamtawala. Ile fimbo ya pembe tatu ambayo alikuwa nayo ni ule ubatizo wa utatu katika majina ya uongo, ndipo kila wakati aanzapo kuinuka kwa kusanyiko kuukubali, yeye humtwanga akamwangusha chini nayo. Na bila shaka, yeye akiwa mkumbwa hivyo, niligeuka—nilikuwa nimemwogopa kidogo, ndiposa nikamvamia hata hivyo, na ile misuli ilikuwa misuli ya imani. Hilo lilinifanya nifikiri, “Kama Mungu yu pamoja nami—anaweza kunipa misuli, hebu nisimame upande wake,” kaacha kumpiga.

Hakuna budi ilikuwa saa nne mchana wakati mke wangu alipokuwa anajaribu kuingia katika kile chumba. Na ikatokea. Niliingia katika ono asubuhi ile na kwa namna fulani mimi . . . Sasa kumbuka haikuwa ndoto!

Kuna tofauti kati ya ndoto na maono. Ndoto ni unapolala. Maono ni wakati uko macho. Tumezaliwa jinsi hiyo. Mwanadamu wa kawaida, anapoota ndoto, iko katika dhamira ya ndani. Na dhamira yake ya ndani iko mbali sana naye. Hisi zake zinatenda kazi, maadamu yeye yuko katika dhamira yake ya kwanza . . . Katika dhamira hii, u mtu wa kawaida. Unaona, unaonja, unahisi, unanusa, unasikia; lakini unapokuwa katika dhamira ya ndani, umelala, wala huoni, huonji, huhisi, hunusi au kusikia. Lakini kuna kitu fulani wakati unapoota kwamba unarudi kwenye dhamira hii. Kuna kumbukumbu ambapo unakumbuka jambo fulani uliloota miaka mingi iliyopita.

Mwanadamu wa kawaida yuko jinsi hiyo. Lakini Mungu anapokusudia awali jambo, hii dhamira ya ndani haipo mbali sana na hapa kwa mwonaji, lakini dhamira zote mbili zipo papo hapo pamoja. Basi mwonaji katika ono haingii usingizini—yeye bado yu macho, na anaona jambo hilo.

Nilikuwa ninawaelezea hayo baadhi ya madaktari hivi majuzi, nao waliinuka na kusema, “Maajabu haya. Kamwe hata hatujafikiria jambo kama hilo.” Nilipokuwa ninapimwa mawimbi, hao walisema hawajaona kitu kama hicho. Vema walisema, “Kuna jambo linalotukia kwako.”

Ndipo nikasema . . . Niliwaambia. Wakasema, “Ndilo hilo, sawa kabisa.”

Unaona, hizo dhamira mbili huwa zimekaribiana sana. Si jambo ningeweza kufanya, na halinifanyi mimi bora kuliko mtu ye yote mwingine. Ni Mungu tu aliyelifanya

hilo jinsi hiyo. Huingii usingizini—uko papa hapa, kama tu umelala. Umesimama hapa ukitazama huko hivi na... ninyi nyote mmeliona, ulimwenguni kote. Huingii usingizini—huku nimesimama hapa kwenye jukwaa nikizungumza na watu. Mnanisikia nikiingia katika maono na kurudi ninapokuwa katika motokaa pamoja nanyi, au mahali pengine po pote, na kuwaambieni mambo ambayo yatatukia. Nalo halishindwi kamwe. Kamwe halijashindwa. Kuna mtu ye yote aliyewahi kuliona likishindwa? La bwana, haliwezi kushindwa. Halitashindwa maadamu ni Mungu. Angalia, papo hapo jukwaani, maelfu, mbele ya makumi elfu ya watu, hata katika lugha zingine ambazo siwezi kuzizungumza —bado halishindwi. Unaona—ni Mungu.

Sasa, katika ono hili, au kama nilipokuwa ninazungumza, niliangalia, nikaona jambo la ajabu. Sasa, ilielekea kana kwamba mwanangu Joseph alikuwa kando yangu. Nilikuwa ninamzungumzia. Sasa, kama utaangalia lile ono kwa makini hasa, utaona kwa nini Joseph alikuwa amesimama pale.

Nami nikaangalia, na palikuwa na kijiti kikubwa. Na katika kijiti hiki katika mkusanyiko wa ndege—ndege wadogo sana, yapata urefu wa nusu inchi na nusu inchi kwenda juu—walikuwa wadogo wa siku nyingi. Manyoya yao madogo yalikuwa yamechakaa. Na kulikuwepo na kama wawili au watatu kwenye tawi la juu, sita au wanane kwenye linalofuatia, na kumi na watano au ishirini kwenye tawi linalofuata—kushuka chini katika umbo la piramidi. Na jamaa hao wadogo—wajumbe wadogo, nao walikuwa wamechoka sana. Nao walikuwa wanaangalia mashariki, nami nalikuwa Tucson, Arizona katika lile ono. Kwa maana ilifanyika makusudi maana Yeye hakutaka mimi nisipate kuona ilikuwa wapi, nilikuwa nikijitoa mbegu zenye miiba za jangwani. Basi nikasema, "Sasa najua hili ni ono, nami najua kwamba niko Tucson. Nami najua kwamba hao ndege wadogo kule wanamaanisha jambo fulani." Nao walikuwa wakiangalia mashariki. Mara tu walipata wazo la kuruka, nao wakaenda upande wa mashariki.

Na mara walipoondoka, kundi la ndege wakubwa likaja. Walionekana kana kwamba ni hua—mbawa zilizochongoka sana, wa kijivujivu hivi, rangi nyepesi zaidi kuliko ambavyo hawa wajumbe wadogo wa kwanza walivyokuwa. Nao walikuwa wakija kasi upande wa mashariki. Na mara tu walipotoweka kwenye upeo wangu wa macho, niligeuka tena kuelekea magharibi, na hapo likatukia. Kukatokea mlipuko ambao kwa kweli ulitikisa dunia nzima! Sasa usikose hili! Na ninyi kwenye kanda, hakikisheni mtalipata hili sawasawa!!

Kwanza mlipuko! Nafikiri ulisikika kama "kizuio cha sauti," au cho chote unachokiita wakati ndege zinapovuka mwendo wa sauti, kisha hiyo sauti inarudi duniani. Ilitikisa tu kama..., ilinguruma, kila kitu! Basi huenda ilikuwa kama sauti kubwa

ya radi na umeme. Sikuona radi. Nilisikia tu ule mlipuko mkuu ambao ulisikika kama wa kutoka kusini toka nilipokuwa; kuelekea Mexico.

Lakini ulitikisa dunia, na ulipoitikisa (nilikuwa bado ninaangalia magharibi), kule mbali katika umilele niliona kundi fulani likija. Ilionekana kama kwamba ilikuwa nukta ndogo. Hazingekuwa chini ya tano, na si zaidi ya saba. Lakini zilikuwa katika umbo la piramidi, kama wajumbe hawa wakija.

Na walipokuja, nguvu za Mwenyezi Mungu ziliniinua juu kuwalaki. Nami naweza kuona . . . hazijaniacha bado . . . siku nane zimepita, na bado siwezi kulisahau. Sijawahi kupata jambo lo lote kunihangaisha kama hilo lilivyonihangisha. Jamaa yangu itawaambieni.

Niliweza kuwaona hao malaika, zile mbawa zilizoelekea nyuma zikienda kasi kuliko sauti ingeweza kwenda. Walitokea Umilele kasi sana kama kufumba na kufumbua jicho. Hakuna muda wa kupepesa jicho lako, pepeso tu. Wakawasili. Sikupata muda wa kuhesabu. Sikuwa na muda, si zaidi ya kungalia tu. Wenye uwezo, malaika wakuu na wenye nguvu, weupe kama theluji! Mabawa yamewekwa kwenye vichwa nao walikuwa "whiu whiiiu," [mlio wa mluzi—Mh.] na ilipotendeka, nilinyakuliwa katika piramidi hii, ya lile kundi. Nikawaza, "Sasa, jambo ndilo hili." Nilikufa ganzi mwili mzima, kisha nikasema, "Loo jamani. Hili linamaanisha kwamba kutakuwa na mlipuko utakaoniva. Nimefikia mwisho wa safari yangu sasa. Yabidi nisiwaambie watu wangu ono hili liondokapo. Sitaki wao walijue, lakini Baba wa Mbinguni ameniacha nijue sasa kwamba muda wangu umeisha. Nami sitaiambia jamaa yangu ili wasiwe na wasiwasi juu yangu, kwa sababu Yeye yu karibu kwenda, Malaika hawa wamekuja kunichukua nami nitauwawa karibuni sasa katika namna fulani ya mlipuko."

Kisha ikanijia, wakati nilipokuwa katika kundi hili, "La, si hilo. Kama ungekuua ungemuua Joseph, na niliweza kumsikia Joseph akiniita." Vema, basi niligeuka tena nikawaza, "Bwana Mungu, ono hili linamaanisha nini?" Nikashangaa, kisha ikanijia. Si sauti—ilinijia tu. Loo! Hao ni Malaika wa Bwana wanaokuja kunipa agizo langu jipya! Na wakati nilipowazia hilo, niliinua juu mikono yangu, nikasema, "Ee Bwana Yesu, wataka nifanye nini?" Basi lile ono likaniacha.

Kwa karibuni saa moja, sikuweza kuhisi.

Sasa, ninyi watu mnajua baraka za Bwana ni nini. Lakini Uwezo wa Bwana ni tofauti kabisa. Uwezo wa Bwana mahali kama hapo, nimeuhisi mara nyingi hapo kabla katika maono, lakini kamwe si namna hiyo. Inasikika kama "hofu ya uchaji." Niliogopa sana mpaka nilikufa ganzi mbele za viumbe hawa. Nasema ukweli. Kama Paulo alivyosema, "Sisemi uongo."

Hamjawahi kunipata nikisema jambo lo lote lisilo sahihi kuhusu jambo kama hilo. Jambo fulani liko karibu kutukia!

Kisha baada ya muda kidogo nikasema, “Bwana Yesu, kama nitauawa, nijulishe ili nisiwaambie watu wangu jambo hili; lakini kama ni jambo jingine, hebu nijulishe.” Hakuna jibu.

Baada ya Roho kuniacha kwa kama nusu saa nadhani au zaidi nilisema, “Bwana, iwapo basi nitauawa, Nawe umemaliza kazi nami duniani, nami nitachukuliwa nipelekwe nyumbani sasa —ambalo kama ni hilo, hilo ni jambo zuri. Hilo ni sawa.” Kwa hiyo, nikasema, “Kama ndivyo, nijulishe. Peleka uwezo Wako juu yangu tena. Ndipo, nitajua sitawaambia watu wangu, au mtu ye yote, kuhusu hilo, kwa sababu uko karibu kuja kunitwaa.” Nami. . .na hakuna jambo lililotukia. Nikangojea kidogo. Kisha nikasema, “Bwana Yesu, iwapo haikumaanisha hilo, na inamaanisha kwamba una jambo nitakalotenda nalo litafunuliwa kwangu baadaye, basi leta uwezo Wako. Basi nusura unitoe mle chumbani!

Nilijikuta mahali fulani pembeni. Niliweza kumsikia mke wangu mahali fulani akijaribu kutikisa mlango. Mlango wa chumba cha kulala ulikuwa umefungwa. Nami nilikuwa na Biblia iliyofunguliwa, ninasoma. . .sijui, lakini ilikuwa katika, naamini, Warumi, sura ya 9, aya ya mwisho: “Tazama naweka katika Sayuni, jiwe la pembeni, jiwe likwazalo, jiwe la thamani la pembeni, na kila amwaminiye hatatahayarika.” Nikawaza, “Ni ajabu ninasoma hilo.” (Roho bado amenishika mle chumbani.)

Nikafunga Biblia na kusimama pale. Nikaenda madirishani, (ilikuwa mnamo saa nne asubuhi, au baadaye) nami nikainua mikono yangu, nikasema, “Bwana Mungu, sielewi. Hii ni siku ng’eni kwangu. Nami karibuni, karibu nirukwe na akili.” Nikasema, “Bwana, hilo linamaanisha nini? Hebu nilisome tena, kama ni Wewe.” (Sasa hili linasikika la kitoto!) Nikaichukua Biblia, na kuifungua. Hilo hapo tena mahali pale pale —Paulo, akiwaambia Wayahudi kwamba walijaribu ku. . .akiwaambia Warumi kwamba Wayahudi walijaribu kulikubali kwa matendo, lakini tunaamini kwa imani.

Vema, umekuwa wakati wa kuogofya tangu hapo. Sasa manaona ninaposimamia. Sijui kinachotendeka! Sijui la kusema! Lakini sasa, hebu mimi sasa, tangu sasa, kwa kama dakika zingine kumi na tano au ishirini, hebu nijaribu kusema kitu hapa sasa. Kumbuka, Hakuna hata wakati mmoja maono yale yameshindwa.

Sasa, nitachukua Maandiko kwa muda mchache. Kama ukiangalia, katika Ufunuo sura ya 10. . .Sasa, hebu niseme hili: Kama hilo ono ni la kimaandiko, linaweza tu kufasiriwa kwa Maandiko. Na halafu nawatakeni muweke hili pamoja. Sasa, ninyi mliopo na ninyi mlio kwenye kanda, hakikisheni

mtasema jambo hili namna ninavyolisema, kwa sababu laweza lieleweke vibaya kwa urahisi sana. (Je! mna haraka? Sawa tu . . . Nawashukuru kwa kuwa kimya jinsi hiyo, na wazuri.)

Sasa yule Malaika wa Saba . . . Sasa, *Je! Mabwana,* (kama nilivyouita huu) *Hii ndiyo Ishara ya Wakati wa Mwisho?* Tunaishi wapi? . . . Ni wakati gani? Kama mshindani mweleka aliyechoka usiku mzima, akiinuka na kugeuza saa aangalie aone ni nini—akiwasha taa. Ombi langu ni, "Mungu tujalie tuiwashe taa!" Ninasimama katika mahali pabaya sana, kama mngelijua tu. Kumbukeni, nawaambieni katika Jina la Bwana, nimewaambieni ukweli! Na jambo fulani liko tayari kutukia! Sijui. Sasa, ninyi mlio kwenye kanda, mnaelewa hilo? Sijui! Nitajaribu—jambo lililonijia jana nikiketi katika chumba changu cha kusomea. Sisemi kwamba hii ni kweli. Ilikuwa tu ni jambo lililosogea moyoni mwangu wakati nilipotembea huku na huko sakafuni!

Nilikusudia kwenda zangu—kuondoka kwa muda kidogo kisha nije huku na Charlie—na kwenda kuwinda naye siku moja, kabla ya kuachana.

Hebu nisema, ati kwamba kwa sababu tu ninaenda Magharibi, siyo kwamba ninaacha maskani haya. Hili ndilo kanisa ambalo Bwana Mungu alinipa. Hapa ndipo makao makuu yangu. Hapa ndipo ninapokaa. Ninaenda tu kwa kutii amri ambayo nimepewa kwa ono. Mwanangu, Billy Paul, ataendelea kuwa katibu wangu. Afisi yangu itakuwa papa hapa kwenye kanisa hili. Kwa msaada wa Mungu, nitakuwa hapa jambo hili litakapomalizika, na kuhubiri zile Muhuri Saba; na kanda yo yote ninasayo, au cho chote kile, itakuwa papa hapa kwenye kanisa hili. Papa hapa, kadiri ninavyojua, ndipo mahali ninapoweza kuhubiri kwa uhuru zaidi kuliko ninavyoweza mahali pengine ulimwenguni —kwa sababu ya kundi la watu hapa wanaoamini na wana njaa na wangali wanashikilia. Ninajisikia nyumbani hapa. Hapa ndipo panapofaa. Na kama ukiangalia, ndoto ile ilizungumzia jambo lile lile. Unaona, ambapo chakula . . .

Sasa, bali sijui kilicho mbele—lakini namjua Ambaye anashikilia wakati ujao. Hilo ndilo jambo muhimu.

Sasa, Mungu, iwapo nimekosea, nisamehe na kifunge kinywa changu, Bwana, kwa cho chote ambacho si mapenzi Yako. Ninatenda hili tu kwa sababu nimechomwa moyo, Bwana. Hebu watu na waelewe— ni kuchomwa moyo tu.

Sababu nafikiri tafsiri haikuja mara moja—ilikuwa uwezo wa Mungu, kwa sababu naamini imeandikwa hapa katika Biblia kwa ajili yangu. Basi kama ni la kimaandiko, ni Maandiko tu yanayoweza kulifasiri. Na kama hili ni kweli, Ndugu, Dada, simaanishi kuwatisha, lakini afadhali tuwe waangalifu sana sasa. Tunakaribia ku . . . jambo fulani liko karibu kutukia.

Sasa, nasema hili kwa unyenyekevu na kicho cha Mungu. Na mnafikiri ningesimama hapa—na ninyi watu hata mnaniamini kuwa nabii. (Sidai kuwa hivyo.) Wazo langu lilikuwa hili. Basi, mwaka uliopita nilisema hili ndilo jambo pekee nililoona, ufufuo umekwisha katika taifa—wa taifa hili kwa vyo vyote. Nilifanya ziara ya kiinjilisti—wengi wenu mlikwenda pamoja nami. Loo, ilikuwa sawa. Tulikuwa na nyakati nzuri sana, mikutano mizuri, halaiki ya watu, lakini haikufua dafu. Mwaka huu ninafanya ziara ya kimishenari. Mara tu nikiweza, nitaondoka niende Afrika, India, na kote ulimwenguni, kama ninaweza, kwenye ziara nyingine ya kimishenari. Kama hilo halitafanikiwa, basi sitakunywa maji wala kula chakula, na nitapanda hiyo milima mirefu kule, nami nitakaa huko, mpaka Mungu anijibu kwa njia fulani. Siwezi kuishi namna hii. Siwezi tu kuendelea. Huenda hili hapa likawa ndilo jibu. Sijui. Mpaka Yeye anibadilishe . . .

Mnakumbuka lile ono, yapata majuma matatu yaliyopita, nikisimama kwenye jua, nikihubiria kusanyiko? Nyote mmekuwa hapa Jumapili iliyopita. Jumapili nyingi ninyi watu hapa mnapata kanda nanyi mpo inaporekodiwa, mnaelewa mambo haya, kwa sababu sasa nitagusia tu sehemu hizi, nanyi liangalieni jambo hilo. Hata tu kila sehemu ya hayo ambayo yamekwisha inalingana kabisa na hili. Kwa hiyo haina budi kuwa tafsiri. Mimi sijui. Hiyo ndiyo sababu ninasema, "Je! Mabwana, jambo hili ndilo?"

Ninaamini kwamba yule Malaika wa Saba wa Ufunuo 10 ndiye Mjumbe wa Wakati wa Saba wa Kanisa wa Ufunuo 3:14. Kumbuka . . . Sasa, hebu nisome . . . angalia . . . ambapo naweza kusoma . . . Sasa, huyu alikuwa Malaika wa Saba.

> *"Isipokuwa katika siku* za *sauti ya malaika wa saba,"* (aya ya 7) " . . . *atakapokuwa tayari kupiga baragumu, hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii."*

Sasa, unaona, huyu alikuwa malaika; naye ndiye malaika wa Wakati wa Saba wa Kanisa, kwa maana inasema hapa, ni Malaika wa Saba wa Wakati wa Saba wa Kanisa. Ukitaka kuona ni nani, au alipo huyo malaika . . . (Ufunuo 3:14). Ni malaika wa Kanisa la Laodikia.

Sasa, mnakumbuka hilo liliponenwa hapo (wale malaika wa Nyakati za Kanisa) . . . Na sasa, katika hili, litafungamana moja kwa moja hata kwenye hizi Muhuri Saba tutakazozungumzia. Basi zile Muhuri Saba ambazo tunajaribu kuzungumzia (tunapokuja wakati huu) ni zile Muhuri Saba zilizoandikwa, na hizi Muhuri Saba, kama mjuavyo, ni udhihirisho wa wale Malaika Saba wa yale Makanisa Saba. Lakini kuna Muhuri zingine Saba ambazo ziko upande wa nyuma wa kile Kitabu—nje ya Biblia. Angalia, tutalifikia hivi punde tu.

Basi, kabla sijaanza hili, je! mmechoka? Mngetaka kusimama, kubadilishana mahali pa kukaa?

Sasa, sikilizeni kwa makini. Yule Malaika wa Saba wa Ufunuo 10:7 ndiye yule Mjumbe wa Wakati wa Saba wa Kanisa. Unaona? Sasa angalia. Katika siku . . . Sasa angalia hapa.

> *Isipokuwa katika siku za sauti ya malaika wa saba, atakapokuwa tayari kupiga baragumu, hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, . . .*

Sasa, kupiga baragumu, mjumbe huyu, Malaika wa Saba hapa, anatangaza ujumbe wake kwa Kanisa la Laodikia. Angalia ujumbe wake ni wa namna gani. Sasa, haikuwa kwa Malaika wa Kwanza, (hakupewa huo), Malaika wa Pili, wa Tatu, wa Nne, wa Tano, wa Sita; Bali ni Malaika wa Saba aliyekuwa na ujumbe wa namna hii. Ulikuwa nini? Angalia, ujumbe wake ni wa namna gani: kumaliza siri zote za Mungu ambazo zimeandikwa katika Kitabu. Malaika wa Saba anamalizia siri zote, zilizolegea, kote katika taratibu hizi na madhehebu —Malaika wa Saba anazikusanya na kumalizia siri yote. Sasa hilo ndilo Biblia imesema —anamalizia siri ya Kitabu kilichoandikwa.

Sasa, hebu na tutazame baadhi ya siri hizi. (Na kama mkitaka kuziandika.) Kwanza, nitachukua ambalo Scofield anasema hapa katika Mathayo 13. Kama ungetaka kunakili baadhi ya hizo . . . Kama huna, Biblia ya Scofield, waweza kusoma ambalo yeye anafikiria baadhi ya siri hizi ni nini.

Sasa, katika aya ya 11:

> Kisha *Akajibu, akawaambia, Ninyi mmejaliwa* . . . "(kwa wanafunzi wake) *Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, bali wao ha—bali wao hawakujaliwa*." (Zile siri).

Siri ni hii. Siri ni maandiko—ukweli uliofichwa hapo kwanza, sasa umefunuliwa Kiungu, bali bado pamebakia jambo la kimbinguni, hata ingawa limefunuliwa. Siri zilizo Kuu zaidi na Siri Kuu ni:

1 Siri ya Ufalme wa Mbinguni. (Hiyo ndio tunayozungumzia hivi sasa. Mathayo 13:3-15.)

Siri ya 2 ni siri ya upofu wa Israeli wakati huu. (Warumi 11:25 ndicho kifungu kinachohusika.)

Siri ya 3 ni siri ya kuhamishwa watakatifu walio hai mwishoni mwa wakati huu. (I Wakorintho 15, na pia I Wathesalonike 4:14-17.)

Siri ya 4, ya Kanisa la Agano Jipya kama Mwili Mmoja, Uliofanyizwa kwa Wayahudi na Mataifa. (Waefeso 3:1-11, Warumi 16:25, na pia Waefeso 6:19, Wakolosai 4:3)

Siri ya 5 ni ya Kanisa, kama Bibi Arusi wa Kristo. (Waefeso 5:28-32.)

Siri ya 6 ni ya Kristo aliye hai, yeye yule jana, leo na hata milele. (Wagalatia 2:20 na Waebrania 13:8, na sehemu nyingi kama hizo.)

Siri ya 7 ni ya Mungu, yaani Kristo, kama utimilifu wa uungu uliofanyika Mwili, ambamo ndani Yake hekima yote ya kiungu na uungu vinarejeshwa kwa binadamu.

Siri ya 9 ni siri ya kuasi inayopatikana katika 2 Wathesalonike, na kadhalika.

Siri ya 10 ni ya Nyota Saba za Ufunuo 1:20. (Ndio tu tumeipitia. Zile Nyota Saba zilikuwa yale Makanisa Saba. Wale Wajumbe Saba, na kadhalika.)

Na siri ya 11 ni siri ya Babeli ya siri, yule kahaba, wa Ufunuo 17:5-7.

Hizo ndizo baadhi ya zile siri ambazo huyu malaika anapaswa kumaliza —siri zote za Mungu. Na ile nyingine—hebu kwa kicho niseme hili na si kunena juu yangu mimi mwenyewe, bali kunena juu ya yule Malaika wa Bwana.

Uzao wa nyoka, ambayo ni siri iliyofichwa kwa miaka mingi.

Neema ikifafanuliwa—si fedheha, bali neema ya kweli na halisi.

Hakuna kitu kama jehanamu inayowaka moto Milele na Milele. Utaungua kwa mamilioni ya miaka, lakini cho chote ambacho kilikuwa cha Milele na Milele hakikuwa na mwanzo wala mwisho, na jehanamu iliumbwa —siri zote hizi.

Siri ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu, bila mshtuko, bali Nafsi ya Kristo ikitenda mle ndani kazi zile zile ambazo Yeye alitenda.

Siri ya ubatizo wa maji, ambapo wale washupavu wa utatu wameuleta katika vyeo vya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na siri ya uungu ikitimizwa katika Ubatizo katika Jina la Yesu Kristo kulingana na Kitabu cha Ufunuo, ambao Kanisa lilipaswa kuupokea wakati huu. Hizo ni baadhi ya zile siri.

Ile Nguzo ya Moto ikirudi. Amina! Hicho ndicho kitu ambacho kinapaswa kutukia, nasi tunaiona!

Loo, jinsi ambavyo tungeweza kuendelea kutaja hizo siri. Kuona ile Nguzo ya Moto ambayo iliwaongoza wana wa Israeli — ile ile iliyompiga Sauli ikamwangusha akienda zake Dameski, na ile ile, ikija na nguvu ile ile, ikifanya mambo yale yale, na ikifunua Neno lile lile, ikidumu neno kwa neno na Biblia.

Kupiga Baragumu humaanisha Baragumu ya Injili. Na kupiga baragumu katika Biblia humaanisha, iweni tayari kwa Vita vya Maandiko. Mnaliandika? Vita vya Maandiko. Paulo alisema . . . (Kama mkitaka kuandika hili, I Wakorintho 14:8.) Paulo alisema, “Kwa maana Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, mtu atajuaje atajitayarishia nini?” Na iwapo haitoi sauti ya maandiko, iliyodhihirishwa, udhihirisho wa Neno

la Mungu ukifanywa wazi, tutaijuaje wakati wa mwisho? Kama inasema wao wanaamini kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele, lakini wanakataa ishara Zake na maajabu ambapo milki yote ya maumbile ilimwamini Yeye, na Kanisa lote lilimwamini Yeye kwa ajili ya hili, tutajuaje jinsi ya kujiandaa?

Mtu fulani anakuja na ramami na akalichora lote, na mtu fulani anakuja na jambo jingine na kuchora hili lote, kinyume cha hili. Mtu fulani aje na kusema, "Ni hili," akirudi kwenye hili, na wengine wameandika vitabu na mambo kama hayo. Bali Mungu huja katika uwezo wa kufufuka Kwake na ni nani atanena dhidi ya jambo hilo? Kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye hutenda vile vile alivyotenda jana, leo, na hata milele. Hilo ndilo malaika huyu anakusudiwa kufanya —kuchukua siri zile, sehemu hizo zilizolegea, ambazo zimewapoteza watu.

Angalia, kama ikitoa sauti isiyojulikana, isiyo ya kimaandiko, nani awezaye kujiandaa? Bali Baragumu... Umeangalia kila moja ya nyakati zile, kama nilivyowaambia kuhusu kuja kwa kanisa, palikuwa na Baragumu iliyolia, Muhuri ukavunjwa; na baragumu humaanisha vita! Kama haitoi sauti ya maandiko, vipi basi? Lakini hebu niwakumbusheni hili. Msilikose sasa.

Angalia, kila wakati wa kanisa ulikuwa na mjumbe wake. Twajua hilo. Paulo alikuwa mjumbe wa kwanza. Na baragumu ya kwanza ilipolia, na Muhuri wa kwanza ukavunjwa, Paulo alikuwa mjumbe wa kwanza kama tulivyoona. Alifanya nini? Akatangaza vita. Juu ya nini? Kanisa la Kiorthodoksi, kwa kutoamini Ishara ya Masihi ambayo Yesu aliwaonyesha.

Mbona, walipaswa waijue! Walipaswa wamjue Yeye!

Kumbuka Paulo alikuja mwishoni mwa ule wakati—wajumbe wote huja mwishoni mwa wakati. Ni wakati wa mwisho wakati ambapo mambo haya yanapoelezwa.

Paulo, akijua Maandiko, na akijua kwamba Yesu alikuwa Masihi, naye akayacharaza yale masinagogi toka mahala hadi mahala kwa Maandiko naye akafukuzwa na kila moja yao. Mpaka mwishowe akakung'uta mavumbi toka kwenye miguu yake na akawageukia Mataifa.

Ilikuwa nini? Kupiga Baragumu! Malaika mjumbe akisimama pale na Neno. Loo jamani! Usikose hilo sasa! Neno! Na Paulo, akiwa na tafsiri isiyoghoshiwa ya Neno la Mungu, alicharaza kila moja ya hayo masinagogi. Ilimgharimu uhai wake.

Jinsi tungeshuka kwenda kwa Ireneo, yule...mjumbe wa wakati wa pili wa kanisa, na Mtakatifu Martini, wakati unaofuatia wa kanisa, walipoanza kupata fundisho la Wanikolai...likaanza kuingia. Nao waliucharaza wakati ule.

Mtakatifu Martini aliucharaza wakati wake. Kisha Luther, mjumbe wa tano, akicharaza Kanisa Katoliki kwa Neno la Mungu. *"Mwenye haki ataishi kwa imani,"* akasema; na "Huu sio ule mwili halisi wa Kristo," na akatupa ule mkate sakafuni, akatoka nje, na akalicharaza hilo Kanisa Katoliki! Hiyo Baragumu ikalia. Hilo ni sawa. Hilo ni sawa?

John Wesley, aliinuka katika siku za Kanisa la Anglikana, waliposema, "Hakuna sababu tena ya kuwa na ufufuo," nalo likapoa kabisa. Lakini John Wesley alisimama na ujumbe wa kazi ya pili ya neema: Utakaso. Naye akalicharaza hilo Kanisa la Kianglikana kwa Baragumu ya Injili —akajiandaa kwa vita. Hilo ni kweli. Alifanya hivyo.

Sasa, tuko katika Wakati wa Laodikia, ambapo wameunda madhehebu tena! Methodisti, Batisti, Presbiteri, Uluteri, Upentekoste, nasi tunangojea kuja kwa nabii, kuucharaza wakati huu, na kuwageuza kutoka kwenye uovu wao.

Sasa, iwapo huo ndio umekuwa mtindo katika nyakati zote, hivi Mungu atabadili mtindo Wake katika siku hii. Hawezi kuubadili. Yampasa ashikilie mwelekeo wa kawaida. Na kumbuka, mjumbe huyu alikuwa Malaika wa Saba, naye alipaswa achukue siri zote na kuzikusanya.

Angalia, Malaika wa Saba alipaswa acharaze hili kanisa tajiri la Laodikia. "Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu." Yeye alisema, "Wewe u mnyonge mwenye mashaka, masikini, kipofu na hujui." Huo ndio uliokuwa ujumbe wake.

Ee Mungu, tupelekee nabii asiye na woga aliye na BWANA ASEMA HIVI ambaye kwake Neno la Mungu lililodhihirishwa litatenda kazi, na kuthibitisha kwamba ametumwa na Mungu. Naye ajapo, atazicharaza nyakati hizo. Hakika atazicharaza. Atalifanya hilo Kanisa la Laodikia limchukie. Hakika litamchukia. Walifanya hivyo katika kila wakati mwingine. Haitabadilika katika wakati huu. Yapaswa iwe vile vile.

Angalia, sasa Kanisa la Laodikia—mjumbe atamaliza wa Laodikia. . . Malaika wa Saba atamaliza siri zote ambazo zimepotezwa katika vita vilivyotangulia kwa ajili ya ukweli.

Luther aliinuka, lakini hakuwa na ukweli wote. Alikuwa tu na kuhesabiwa haki. Sawa! Hatimaye akaja mjumbe mwingine aliyeitwa John Wesley akiwa na utakaso. Hakuwa nao. Biblia ilisema. . . Kanisa la Filadelfia. Kisha ukaja Wakati wa Kanisa la Laodikia na Ubatizo wa Roho, lakini waliuchafua wote na wakarudi kwenye desturi kama hao walivyofanya mara ya kwanza —ambapo Yeye alipoonekana kama Alfa na Omega. Mkono Wake ukiwa upande mmoja, na upande mmoja—wa kwanza na wa mwisho.

Roho Wake alishuka kwenye siku ya Pentekoste na kulijaza kundi hilo. Pole pole kanisa lilikauka, mpaka likapitia Nyakati

za Giza, Vile Vinara Saba vya Dhahabu, Nyakati Saba za Kanisa. Wa mwisho ulikuwa mbali sana Naye. Hiyo ilikuwa karibu miaka elfu moja—miaka elfu moja ya Nyakati za Giza la Kanisa la Katoliki. Lutha akaanza kuleta Nuru inayofuata, karibu kidogo na Neno. Nuru iliyofuata, karibu zaidi kidogo. Nuru iliyofuata, Laodikia, ndipo ikarudi nyuma moja kwa moja kama ilivyofanya mara ya kwanza. Ilirudi moja kwa moja kwenye mchafuko ule ule wa mara ya kwanza. Huoni ninalomaanisha?

Sasa angalia. Kuna ukweli mwingi uliopotezwa kule. Kwa nini? Ambapo wengine walipatana juu ya ukweli. Lakini huyu Malaika wa Saba hapatani kwa cho chote! Anakusanya sehemu zote zilizolegea —anazikusanya, zote na anapopiga baragumu, siri zote za Mungu zingemalizika. Mungu alimtuma. Siri zote zilizofichwa zilimalizika wakati yeye. . . Ilifunuliwa kwake. Na nini? Iwapo hizi ni siri zilizofichwa, mtu huyo atatapaswa kuwa nabii. Na je! hatukupitia na kuona kwamba nabii atakayekuja katika siku za mwisho angekuwa yule Eliya mkuu ambaye tumekuwa tunamtazamia? Kwa sababu siri hizi ambazo zimefichwa kwa wanatheolojia zitapaswa kufunuliwa kupitia kwa Mungu, na Neno huja tu kwa nabii. Nasi twajua hilo. Yeye atakuwa Eliya wa pili, kama ilivyoahidiwa. Loo, jamani! Ujumbe atakaoleta utakuwa siri zile za mambo yote haya.

Tuna ubatizo wa maji—wote umevurugika. Hiyo ni kweli. Mmoja ananyunyizia maji, mmoja anamwagia maji, mmoja anachukua Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, mmoja anachukua hili, mmoja anabatiza mara tatu kifudifudi—mara moja kwa Mungu anayeitwa "Baba," na mara nyingine kwa Mungu anayeitwa "Mwana," na mara nyingine kwa Mungu anayeitwa "Roho Mtakatifu." Mwingine husema, "Mmekosea, yawabidi kubatiza kichalichali mara tatu namna hiyo"—na loo, mchafuko jinsi gani! Lakini jambo lote limekusanywa tayari! Kwa maana kuna Mungu mmoja tu! Na jina Lake ni Yesu Kristo, na hakuna jina jingine chini ya Mbingu. . . Hakuna fungu moja la Maandiko, mahali po pote katika Biblia, ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa kwa namna nyingine isipokuwa katika Jina la Yesu Kristo. Hapana hata wakati mmoja ye yote wa kanisa jipya. . . au wa Kanisa la Yesu Kristo aliwahi kunyunyiziwa, kumwagiwa maji, au cho chote kile. Hapana hata wakati mmoja imewahi kutumiwa ibada, "Nakubatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Ni kanuni za imani na mambo mengineyo. Na katika vita vya ukweli, hivyo visehemu vilivyolegea vimepotezwa; lakini Mungu alisema vingerejeshwa tena katika siku za mwisho. *"Nitawarudishia,!* asema Bwana." Tulipitia hilo si muda mrefu uliopita katika "Mti wa Bibi Arusi."

Itahitaji nabii. Biblia inasema kwamba atakuja. Hilo ni kweli. Malaki 4 inasema kwamba atakuja, nasi tunaamini kwamba atakuja. Tunamtazamia, na tunangojea kudhihirika kwake. Nasi tutaona Neno la Mungu lililothibitishwa.

Ni wachache tu watakaoelewa hilo. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Kuliokolewa nini? Watu watano. Katika siku za Lutu, waliokolewa hasa watatu. Mkewe alianza naye akapotea. Ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu. Ni wachache sana watakaookolewa—watakaohamishwa wakati ule. Mojawapo ya zile siri ni lile Kanisa likitwaliwa—kama Lutu alivyotwaliwa—kama Lutu alivyotwaliwa. Nuhu alitwaliwa, na Kanisa litatwaliwa pia. Mmoja aliingia, mmoja akatoka, na mwingine atapaa juu. Unaona ni sawa kabisa, kikamilifu. Neno huja.

Kitabu kile kilichoandikwa ndani basi kinamalizwa, wakati siri hizi zote zimekwisha kutangazwa.

Sasa, hebu nilisome tena, ili muwe na hakika. Sasa tazama: *"Isipokuwa katika siku za malaika wa saba,"* (malaika wa mwisho) *"atakapokuwa tayari kupiga baragumu, hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa . . . "*

Sasa, siri ya Mungu ni nini . . . mojawapo? Paulo alisema katika I Timotheo 3 (naamini ndipo) Alisema, *"Bila shaka siri ya uungu ni kuu . . . "* Maana Mungu alidhihirishwa katika mwili. Tulimshika, tulimuona Yeye, akapokelewa juu kwenye utukufu. Akashuhudiwa na malaika, akathibitishwa hapa duniani—Mungu alithibitishwa.

Hakika, ni siri kuu, bali yote imetatuliwa. Si Baba, Mwana na Roho Mtakatifu—Mungu watatu, bali Mungu Mmoja katika afisi tatu. Ubaba chini ya Musa, Uana chini ya Kristo, Roho Mtakatifu chini ya wakati huu. Nyakati tatu za Mungu yule yule—si Mungu watatu.

Siri imekwisha sasa. Biblia ilisema ingekwisha.

Wakati wao—nimeona hivi majuzi ambapo wanasayansi wanajaribu kunipinga katika kile walichokuwa wakisema. Niliposema, "Mtu ye yote ambaye ameamini kwamba Hawa alikula tofaa!" Sasa, sayansi inasema, (niliona katika gazeti hivi majuzi kwenye kichwa cha maneno) alikula embe dodo. Upuzi! Hilo lingemdanganya? La hasha. Unaona, wao . . . Hilo ndilo Kaini alifikiria, wajua. Alirudisha kitu kile kile, bali Mungu hakuitakabali sadaka yake; na Habili, mwenye haki, ilifunuliwa kwake kwamba ilikuwa damu, naye akaleta damu. Loo Mungu, Kanisa hili na wakati tunaoishi!

Kitabu kilichoandikwa upande wa ndani basi kinamalizika wakati malaika huyu akomapo—sasa tafadhali eleweni hili!—wakati ujumbe wa Malaika wa Saba umalizikapo—siri za uungu, siri ya uzao wa nyoka, siri zote zingine za mambo haya yote—uana wa milele, kama wanavyozungumzia. Yeye awezaje awe mwana wa milele, na huku umilele haukuanza kamwe wala hauna mwisho? Na mwana ni kitu ambacho kinazaliwa. Yawezaje kuleta maana?

Yawezekanaje kuwe na Jehanum ya milele, na huku Jehanum iliumbwa? Ninaamini katika Jehanum inayowaka moto. Hakika. Biblia ilisema hivyo, bali ni kwa ajili ya kuharibu. Biblia ilisema, "Heri ni yeye ambaye hana fungu katika mauti ya pili." Unaona? Unaona, hutaharibiwa na mauti ya pili. Ya kwanza ni ya kimwili. Ya pili ni kifo cha kiroho wakati kila kitu kimekwisha. Nafsi itendayo dhambi; nafsi hiyo itakufa. Utaadhibiwa kwa dhambi zako, labda kwa mamia ya maelfu ya miaka, lakini hakuwezi kuwa na Jehanum ya milele, kwa sababu Biblia ilisema Jehanum iliumbwa. Yawezaje kuumbwa na iwe ya Milele? Iwapo kuliwahi kuwa . . . Biblia ilisema Jehanum iliumbiwa shetani na malaika zake. Basi iwapo iliumbwa, haiwezi kuwa ya Milele; kwa sababu Milele . . . cho chote cha Milele hakijawa na mwanzo wala kuwa na mwisho.

Hivyo ndivyo ambavyo hatuwezi kufa kamwe, kwa sababu tulikuwepo daima. Tu sehemu ya Mungu. Uzao wa Mungu. Na Yeye ndiye kitu pekee cha Milele kilichopo, amina. Huwezi kufa kuliko Mungu awezavyo kufa, kwa sababu wewe u wa Milele pamoja Naye. Amina! Hebu na lije. Haleluya! Nimechoka kwa namna fulani na nyumba hii ya kale ya maradhi kwa vyo vyote.

Angalia, Kitabu kile kimeandikwa. Wakati Malaika huyu amalizapo siri hizi zote zilizolegea ambazo katika vita walimpiga vita Luther, vikapiganwa katika Wesley, vikapiganwa katika Wapentekoste, vikapiganwa . . . lakini yuaja mmoja, Biblia inasema, kwamba katika siku zake za kupiga baragumu, siri zote hizi . . . Waumoja walienda kando katika Jina la Yesu. Wautatu walienda kando kwenye Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, kama tu walivyotenda kwenye Baraza la Nikea. Jambo lile lile. Wote wawili walikosea. Lakini sasa, katikati ya barabara, ukweli umo katika Mandiko. Unaona mahali tulipo? Malaika wa Bwana.

Angalia, Ufunuo 5:1. Sikiliza hili sasa.

> *Kisha nikaona katika mkono wa kuume wake Yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi kitabu kilichoandikwa ndani"* (maandishi yalikuwa ndani) *"na nyuma, kimetiwa muhuri saba."*

Sasa kuna maandishi ndani ya Kile Kitabu, lakini upande wa nyuma kulikuwa na Muhuri Saba nyuma yake ambazo hazikuandikwa katika kile Kitabu. Sasa, huyu ni mfunuzi anayezungumza—Yohana. Sasa kumbuka, haikuandikwa katika kile Kitabu, "Na katika siku za sauti ya Malaika wa Saba siri yote ambayo imeandikwa ndani itakapotimizwa." Itashughulikiwa katika siku ile.

Sasa mnaona ninalomaanisha? Mnanifuata?

Basi wakati umewadia wa kufunuliwa kwa Sauti zile Saba za Ufunuo 10. Kitabu kile kimalizikapo, kuna jambo moja tu limesalia, na hilo ni zile Sauti za siri za Ngurumo Saba

zilizoandikwa nyuma ya kile Kitabu ambazo Yohana alikatazwa kuandika. Hebu nisome hilo.

> *"Kisha nikaona malaika mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, amevikwa wingu: na upinde wa mvua juu ya kichwa chake, na uso wake ulikuwa kama jua, na miguu yake kama nguzo za moto.*
>
> *Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa:"* (mnaona, sasa angalieni hili) *"akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi.*
>
> *Naye akalia kwa sauti kuu, kama simba angurumavyo: na alipolia, ngurumo saba zikatoa sauti zao."*

(Angalia!)

> *"Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao, nalikuwa tayari kuandika."*

(Kulikuwa kumenenwa kitu. Haikuwa ni kelele tu. Kitu fulani kilinenwa. Alikuwa tayari kuandika.)

> *"Nami nilisikia sauti kutoka mbinguni ikisema,"*

(Angalia mahali zile sauti zilikokuwa katika zile Ngurumo—si Mbinguni, Nchini! Zile Ngurumo hazikutoa sauti kamwe toka mbinguni, zilitoa sauti toka Nchini.)

> Nami *"Nalikuwa tayari kuandika: wakati niliposikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Yatie muhuri . . . "* (Herufi kubwa M-U-H-U-R-I) *"Yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo ngurumo saba, usiyaandike."*

(Iko upande wa nyuma.) Kitabu kimalizikapo . . . Sasa Yeye hakusema upande wa mbele, Yeye alisema upande wa nyuma. Baada ya yote kumalizika, ndipo Ngurumo hizi Saba, sauti, ndicho kitu pekee kilichobandikwa kwenye kile Kitabu, ambacho hakijafunuliwa. Hata hazikuandikwa katika kile Kitabu.

Loo, jamani! Laiti ningewaelewesha watu jambo hilo na ningeweza kweli . . . Msikose, msikose, tafadhali msikose wakati huu. Niko karibu kuwaacheni. Msikose! Kama mliwahi kusikiliza, sikilizeni. Muhuri hizi ziko nyuma ya kile Kitabu, na wakati yule Malaika wa Saba atakapopiga baragumu, siri zote ambazo zimeandikwa katika Kitabu zimekamilishwa. Na mara tu, Kitabu ambacho kilikuwa kimefunguliwa na kuandikwa ndani, kinafungwa! Siri za Mungu zimetimizwa; na hizi ndizo siri za Mungu —kunyakuliwa kwa Kanisa, na mambo haya yote mengine. Siri zimekwisha.

Wakati yule malaika wa saba anapiga baragumu ya kila siri, imekwisha. Hata awe nani. Hata iwe nini. Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Naye alisema,

> *"Isipokuwa katika siku za malaika wa saba, atakapokuwa tayari kupiga baragumu, hapo ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake manabii."*

Mambo yote yale. Kama Rumi kuwa kahaba, na makanisa yote haya ya Kiprotestanti, madhehebu, yakiunda madhehebu kama yake, yamekuwa makahaba wake. Unaona? Siri hizo zote ambazo manabii wamezinena habari zake zitafunuliwa papa hapa katika saa hii ya mwisho. Na wakati Malaika huyu wa Saba anapoinuka katika Wakati wa Laodikia na kuanza kupiga Baragumu ya kweli . . . Kwa sababu itahitilafiana, hawataiamini. Hakika hawataiamini. Lakini atakuwa nabii mwenye upako, kwa sababu hakuna njia ya kuliwazia. Binadamu anajaribu kuwazia utatu hata anapata mvi na kushikwa na wazimu. Hakuna awezaye kulielewa. Wangali wanaamini Hawa alikula tofaa, na mambo yote hayo. Kwa sababu ni mapokeo ambayo binadamu ameshikilia, kama tu Yesu alivyolikuta kanisa. Lakini itabidi iwe nabii anayeongozwa Kiungu apate kujiliwa na Neno la Mungu na tafsiri ya kweli ya ufunuo wa Yesu Kristo! Kwa hiyo hilo lapaswa kuwa namna hiyo! Mungu atusaidie.

Sasa anapopiga baragumu . . . Sasa hilo ni BWANA ASEMA HIVI! Tunapata hilo wazi. Anapotangaza ujumbe wake—anatangaza vita—kama Paulo alivyofanya kwa wale wa Kiordhodoksi, kama wengine wao walivyofanya, kama Luther, Wesley—dhidi ya madhehebu, wakati atangazapo vita na kuwaambia kwamba wanadanganya na siyo ukweli, na wanawadanganya watu, anapopiga baragumu hiyo, huwezi kukosea, haitashindwa, kwa sababu atathibitishwa na Neno la Mungu. Mtajua ni nini hasa. Naye akifanya hivyo, atapiga baragumu kuitana watoke Babeli, "Tokeni kwake enyi watu wangu na msizishiriki dhambi zake." Mungu na ampeleke—msilikose.

Sasa, aanzapo kupiga baragumu, siri itatimizwa. Sasa, angalia: Basi wakati umewadia wa kufunuliwa kwa zile Sauti za Muhuri Saba za Ufunuo 10. Mnaelewa? Wakati siri zote za kile Kitabu zimemalizika, na Biblia ilisema hapa kwamba angetimiza zile siri. Wakati watu kule katika nyakati zingine wamepigania ukweli; walipigania kuhesabiwa haki; wanashangaa kwa nini kutakaswa, walipigania hili, na walipigania lile, walipigania hili . . . Walifanya nini? Waligeuka moja kwa moja na kufanya madhehebu katika jambo hilo. Jambo lile lile—Wapentekoste, Wabatisti, Wapresbiteri, Waluteri—kila mmoja alitenda jambo lile lile—wakageuka kabisa na kutenda jambo lile lile. Na Biblia ilisema katika Ufunuo 17 hilo ndilo ambalo wangetenda. Mama kahaba wa kale na binti zake—Babeli wa siri.

Biblia ilisema hapa kwamba hilo lingekuwa mojawapo ya zile siri ambazo zingefunuliwa. Waprotestanti—makahaba,

wakitenda uasherati wa kiroho, wakiwaongoza watu kwa madhehebu yao na kikombe chao cha maovu ya fundisho la kutungwa na binadamu, na kuwavuta kuwaondoa kwenye chemchemi iliyojaa Damu ambapo uwezo wa Mwenyezi Mungu humiminika mfululizo kumdhihirisha Yesu Kristo!

Iwapo hiyo ni kweli, basi Mungu ataliunga mkono; Naye amekwisha litenda; Naye ataendelea. Lakini wakati hilo litakapotimia, Neno limekamlishwa.

Sasa, kuna kitu kimoja tu kimebakia. Hicho ni Zile Ngurumo Saba ambazo hatuzijui; na isingelinguruma bure. Mungu hatendi jambo kimchezo. Sisi hucheza na kutenda kipumbavu, lakini si Mungu. Kila kitu kwa Mungu ni ndiyo na siyo. Hachezichezi. Hadanganyi. Humaanisha asemayo, na Yeye haneni jambo lo lote isipokuwa lina maana.

Nazo Ngurumo Saba papa hapa katika ufunuo, hapa, wa Yesu Kristo, ni siri fulani. Biblia haisemi kwamba huu ni ufunuo wa Yesu Kristo? Vema, kuna siri fulani yake iliyofichwa . . . ? . . . ! Ni nini? Zile Ngurumo Saba zina hiyo siri. Kwa maana Yohana alikuwa tayari kuandika, na sauti ilishuka kutoka Mbinguni ikasema, "Usiliandike. Bali litie muhuri; litie muhuri. Liweke kwenye upande wa nyuma wa kile Kitabu." Lapaswa lifunuliwe. Ni zile siri.

Sasa, tumeyatatua mambo haya kwa Roho Mtakatifu. Alituambia hayakuwa matofaa; ilikuwa kujuana kimwili. Alituambia mambo haya. Hakuna mtu awezaye kusimama mbele yake. Sijawahi kuona mhubiri maishani mwangu aliyekubaliana nalo. Lakini nimewauliza . . .

Mnajua huko Chicago, hapo tuliposimama mbele yao, yapata wahubiri 350 . . . (Ninyi wanawake hapa kutoka Chicago, mlikuwepo pale nanyi mlilisikia.) Naye Bwana aliniambia siku tatu kabla. Yeye alisema, "Watakutegea mtego." Akasema, "Simama dirishani, nami nitakuonyesha." Kasema, "Bw. Carlson na Tommy Hicks watakutana nawe kesho asubuhi na wakitaka mwende kula kiamshakinywa, nawe mwambie Tommy asiende." Lakini," Yeye akasema, "hivi ndivyo itakavyoonekana: Waambie kwamba hawataufanyia huo mkutano katika mahali wanapofikiria. Watakuwa mahali pengine." Kasema, "Usiogope, nitakuwa pamoja nawe." Hilo ni sawa kabisa kwangu.

Asubuhi iliyofuata Bw. Carlson, rais wa Wafanyi Biashara wa Injili Yote, akaja . . . kasema . . . kaniita akasema, "Ndugu Branham, nataka twende tukale kiamshakinywa pamoja nawe."

Nikasema, "Sawa." (Nikasema, "Tazama Tommy Hicks atakuwepo pia.")

Tukashuka kwenda huko Town and Country, naye akasema, "Vema, Ndugu Branham, loo hili ni ajabu . . . "

Nikasema, "Tommy, utanifanyia fadhili?" "Hakika, Ndugu Branham."

Nikasema, "Hivi usingenena kwa niaba yangu?"

Akasema, "Loo, si—singeweza kufanya hilo."

Nikasema "Kwa nini? Mimi ni mwanafunzi wa darasa la saba tu na ni-ningesema *empire* badala ya *umpire*. Unaona? Sijui namna ya kuzungumza mbele yao, na kutakuwa na Chama cha Wahudumu wa Greater Chicago. Nitazungumzaje mbele yao na elimu yangu ya darasa la saba, Tommy? Wewe u Daktari wa Dini." Nikasema, "Ungejua jinsi ya kuzungumza, mimi sijui."

Akasema, "Ndugu Branham, nisingeweza kufanya hilo."

Nikasema, "Kwa nini? Mimi nimekutendea wewe fadhili nyingi." (Nililiweka sawasawa kweli.)

Naye Ndugu Carlson akasema, "Loo Ndugu Branham, asingeweza kufanya hicho."

Nikasema, "Kwa nini?"

Akasema, "Vema . . . duh . . . duh . . . hicho . . . aa."

Nikasema, "Mnajua kwa nini? Mnajua kwa nini, bali hamtaki kuninambia. Wamenitegea mtego." Nikasema, "Ndugu Carlson, mmepata chumba kile cha hoteli, sivyo, ambapo tulifanyia karamu ile?"

"Ndiyo."

Nikasema, "Hamtakipata."

Akasema, "Vema Ndugu Branham, tumekwisha kukiwekea rehani."

Nikasema, "Sijali mlivyofanya, hakitakuwepo. Hicho ni chumba cha rangi ya kijani. Tutakuwa kwenye chumba cha rangi ya kahawia. Nitakuwa pembeni. Dkt. Needle ataketi kulia. Yule mtu mweusi na mkewe wataketi hapa, na fulani na fulani. Kasisi wa Kibudha ataketi mwisho kabisa wa mkono wangu wa kulia, na jinsi watakavyokuwa wamevaa." Kisha nikasema, "Unajua ni nini, Tommy. Wewe ni wa Chama cha Wahudumu wa Greater Chicago watashindana nami juu ya Ubatizo katika Jina la Yesu Kristo! Chama cha Wahudumu wa Greater Chikago kitashindana nami juu ya uthibitisho wa Roho Mtakatifu kunena kwa lugha! Watashindana nami juu Uzao wa Nyoka, na juu ya kuhubiri neema."

Tommy akainua macho akasema, "Mama wee." Akasema, "Sidhani nitakwenda."

Nikasema, "Ndiyo, njoo."

Kesho yake, yule mtu aliyechukua rehani, akamrudishia hiyo rehani, akasema "Tuna taarabu. Kilikuwa kimeagiziwa na tulisahau na kupoteza jambo hilo; nasi ilitubidi kukitoa kwa

taarabu, nanyi hamwezi kukipata." Nasi tukatoka kwenda huko Town and Country.

Kaingia asubuhi ile, na hapo wote walisimama. Nilipoketi nyuma ya dawati, huko nyuma, nikingojea, baada ya wao kula kiamsha-kinywa, niliwaangalia kila upande hivyo, (Tulikula kiamshakinywa kwenye chumba, tukatoka, tukaketi) na hapo kilikuwepo Chama cha Wahudumu wa Greater Chicago. Nikawaangalia kila upande. Kila mmoja alijitambulisha mwenyewe kama Daktari Ph.D., LL., "Q.U.S.T." na vitu kama hivyo. Niliketi tu na kuwasikiliza.

Hata wakamaliza. Basi Ndugu Carlson akasimama. Akasema, "Mabwana . . . " (Na ninyi nyote mnajua Hank Carlson. Mbona, tunayo kwenye kanda papa hapa. Iwapo mnataka kununua hiyo kanda ipo hapa. Wavulana wanayo.) Akasema, "Mabwana . . . " Akasema, "Nawajulisheni anayefuatia, Ndugu Branham." Akasema, "Nyote huenda msikubaliane naye katika mafundisho yake, lakini hebu niwaambieni jambo fulani: Siku tatu zilizopita tuliketi mahali fulani, na kama mtu huyo hakuniambia kila kitu kilichotukia asubuhi hii, mimi sisimami hapa. Aliniambia kwamba ninyi nyote mlikuwa mmejiandaa kumswali juu ya mafundisho yake, naye aliniambia ingenibidi kuacha mahali hapo pengine kisha tuje hapa, na aliniambia wapi hasa Dkt Mede, na watu hawa wangeketi wapi, sawasawa kabisa tu, nao hawa hapa." Akasema, "Mnaweza msikubaliane naye, lakini nawaambia jambo moja, yeye ni jasiri kwa yale anayowazia." Akasema, "Sasa, Ndugu Branham, ukumbi ni wako."

Nikasema, "Kabla ya kuanza, (nilisoma nililosoma asubuhi hii, Sikuyaasi Yale Maono Ya Mbinguni.) Nikasema, "Sasa hebu na tuyamalize haya. Sasa, ninyi nyote mnazungumzia kuhusu kuwa Madaktari wa Dini, na mimi ninasimama hapa peke yangu". Nikasema, "Kama hivyo ndivyo, mnataka kunihoji juu ya Ubatizo katika Jina la Yesu—tutaanza na hilo kwanza. Nataka mmoja wenu enyi watu alete Biblia yake asimame hapa kando yangu, juu ya jambo lo lote ambalo nimefundisha." Nikasema, "Asimame hapa kando yangu! Na kwa Neno la Mungu, alikanushe." Nikangojea, na hakuna mtu aliyesema cho chote. Nikasema, "Ninataka mmoja wenu ninyi watu aje asimame kando yangu." Kasema, "Mna nini lakini? Basi msinisumbue, kama mnaogopa kusimama hapa kando yangu." Hawaniogopi mimi. Ni yule Malaika wa Mwenyezi Mungu, ambaye wanajua kama Yeye anaweza kutabiri kuja kwangu mimi, walijua . . . Walikuwa na akili kuliko nilivyofikiria. Wasigethubutu kusimama hapo.

Mwajua mmekuwa katika nyakati . . . nyakati kama hizo pia, lakini hawakulitenda. Kuna shida gani? Kama ni jambo kuu namna hiyo nao wanajua ni la kweli . . . Naliliweka kwenye kanda, na mahali pengine po pote niko tayari kulizungumzia

kwa namna ya Kikiristo na ndugu ye yote. Sitabishana na mtu ye yote, bali nawataka mje mlibatilishe lo lote la mambo hayo—kwa Neno —sio kwa vitabu vyenu sasa, siyo ambalo Daktari fulani na fulani, au Mtakatifu fulani au fulani, alivyosema. Nataka kujua ambacho Mungu amesema. Huo ndio msingi wake. Nataka kujua hilo ni nini. Hawafanyi hivyo.

Sasa angalia, unapowadia wakati wa Sauti zile Saba (na wakati wa zile Sauti Saba unawadia kile Kitabu kinapomaliziwa) za Ufunuo 10 kufunuliwa. Sasa angalieni, sikilizeni. (Sasa sitawaweka kwa muda mrefu zaidi, najua ninawachosha hapa; ni saa nne kasoro dakika ishirini). Sikilizeni kwa makini, sasa. Najua mnasimama nanyi mnabadilishana mahali pa kuketi na kadhalika. Nitafurahi wakati kanisa litakapomalizika kusudi tusisongane sana. Twaweza kuchukua siku nzima kuzihubiri.) Sasa angalieni. Sasa tazameni, zile Sauti Saba zilikuwa Ngurumo—Mshindo!

Mungu atusaidie! Kama nimekosea, Bwana anisamehe.

Ninawaulizeni ninyi swali. Kulikuwa na mshindo wa Ngurumo, sauti hii ilipovuma. Mlitambua hilo wakati zile Muhuri Saba, ambazo zilifuata Wakati wa yale Makanisa Saba—Muhuri ya Kwanza ilipofunguliwa, kwamba kulikuwa na Ngurumo? Muhuri ya Kwanza katika kile Kitabu ilipofunguliwa, kulikuwa na Ngurumo. Je! Muhuri ya Kwanza kwenye upande wa nje wa Kitabu kile isingefunguka kwa njia ile ile? Mungu habadilishi mpango Wake.

Hebu tufungue Ufunuo 6.

> *"Kisha nikaona hapo Mwana-Kondoo alipofungua moja ya zile muhuri, nikasikia mmoja wa wale wenye uhai wanne akasema, kama kwa sauti ya ngurumo, Njoo!"*

Sasa, hapakuwepo kamwe na Ngurumo nyingine; na muhuri ya mwisho ilipofunguliwa, pakawa na kimya Mbinguni kwa muda wa nusu saa. Lakini Muhuri ya Kwanza ilipofunuguliwa, kulikuwa na mshindo wa Ngurumo.

Loo kanisa, ingewezekana? Tuko umbali huo? Marafiki, fikirieni! Pengine . . . , natumaini sivyo, bali je! vipi kama ndivyo ilivyo? Mshindo ule ulikuwa nini? Na mbele ya Mungu na Biblia hii iliyofunguliwa, sidanganyi! Mshindo ambao uliitikisa dunia. Na wakati Muhuri ya Kwanza ya zile Saba ambayo ilifunguliwa katika Biblia, ukatokea—mmoja tu—bali mshindo ambao ulitikisa kitu hicho chote. Ngurumo. Basi, iwapo zile Mihuri zilizoko upande wa nyuma zingefunguliwa, je, isingekuwa Ngurumo pia? Sijui. Siwezi kusema.

Palikuwa na Ngurumo. Muhuri ya Kwanza. Na ile Muhuri ilikuwa Ngurumo, Baragumu ilifunguliwa wakati ule, na Baragumu ilipigwa hapo Pentekoste, bila shaka. (Sitaingilia hilo.)

Sasa, iwapo lile ono lilikuwa la kimaandiko, (ono ambalo ninalizungumzia, ambalo nililiona Jumamosi iliyopita asubuhi—wiki moja iliyosasa). Iwapo, sasa kumbukeni hapa, iwapo lile ono lilikuwa la kimaandiko, yabidi lifasiriwe kwa Maandiko, au maendelezo ya Andiko lile lile! (Nilingojea tu hilo lizame ndani.) Kama hili ambalo nimeona... Sijui ilikuwa ni jambo gani, lakini nimeogopeshwa kupindukia! Hivi tumekwisha? Hivi tuko mwisho? Kumbuka, Malaika huyu alisema kwamba hili litukiapo, Yeye aliapa hapatakuwa na wakati baada ya haya. Nashangaa kama kweli tunalielewa hili?

Unasema, "Vyema inaonekana kana kwamba ingetoa kishindo kote..." Ndugu, Yeye yuaja katika dakika usiyodhania. Utalisikia wakati wako wa mwisho.

Sasa, iko wazi? Muhuri ya Kwanza ilipofunguliwa—Muhuri ambayo ilikuwa ndani ya kile Kitabu, Siri hizi ambazo zilikuwa zikitangazwa—Kuhesabiwa haki, Utakaso, Kanisa Katoliki la Kirumi, Waprotestanti, na hapo vita vyao vyote vidogo na kadhalika vilipoacha mambo haya yaliyolegea katika Neno la Mungu, yule Malaika wa Saba anakuja na kuyakusanya yote na kuyaelezea. Unaona? Na basi anapomalizia, zile Ngurumo Saba zinatoa sauti! Naye Yohana akaanza kuandika. Akasema, "Usiliandike, bali litie muhuri." Na Muhuri ya kwanza ilipofunguliwa ya zile Muhuri zilizo ndani ya kile Kitabu; ilifunguliwa kwa Ngurumo.

Iwapo hili ni Maandiko, yaweza tu kuwa... Kama Andiko lo lote ni jambo lo lote ambalo lapaswa kuwa la Biblia... Ni kama tu usivyoweza kuniambia kuna kitu kama pargatorio na mambo kama hayo. Hakuna Andiko katika Biblia la kuiunga mkono.

Huwezi kuniambia kuhusu mambo haya kama Kitabu cha Makabayo, ambacho chaweza kikawa ni sawa, na kile Kitabu cha nne cha Danieli, ambapo Malaika alimshikia kwenye nywele za kichwa na kumketisha chini. Hakuna upuzi kama huo uliowahi kutukia katika Biblia—ambapo Yesu wa Nazareti alitengeneza ndege mdogo wa udongo wa mfinyanzi, na kumwekea miguu, akasema "Ruka uende zako ewe kijindege"—ni upuzi. Hakuna cho chote katika Biblia kinachounga hicho mkono.

Kwa hiyo haipumbazi... Wafasiri—Mungu alihakikisha kwamba wafasiri hata hawakuongeza fundisho hilo la sharti na upuzi. Yawezekana walikuwa watu wazuri, ndugu wa Makabayo kwa maana... Sisemi hawakuwa watu wazuri, lakini halikuwa la kimaandiko. Huu ni Ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Hakuna cho chote kingeweza kuongezewa Kwake, au kuondolewa Kwake. Na kama tukiweka hilo hapo ndani, halipatani na Maandiko mengine. Kuna vitabu 66 vya Biblia hii, na hamna hata neno moja litapingana na lingine!

Basi kama hii ni kuendelezwa kwa kupigwa kwa Baragumu hizi za mwisho au hizi Ngurumo Saba za mwisho ambazo zinakuja—zile Siri, ule Muhuri wa mwisho, itabidi ushindane au ulingane na Maandiko mengine. Na kama hizo za kwanza hapo zilifunguliwa kwa mshindo wa ngurumo, za pili pia, hizo zilizo upande wa nyuma.

Angalia linalotukia. Kama hilo ono lilikuwa ni Maandiko, basi labidi lifasiriwe kwa Maandiko, au kuendelezwa kwa Andiko lile lile.

Angalia, Ufunuo 3 na 4. Ngurumo Saba . . . Zile Ngurumo Saba! Na basi angalia . . . (3-4). Na nini basi? Kiapo cha huyo Malaika mwenye nguvu kwamba wakati umekwisha. Wakati Ngurumo hizi, unaona, zilipotoa Sauti zao, basi yule Malaika . . . Hebu fikiria tu hilo—Malaika aliyevaa wingu, na upinde wa mvua umefunika kichwa Chake, (Vema, mwajua huyo ni nani!) akaweka mguu mmoja katika nchi na katika bahari na akainua mkono Wake akaapa kwamba Ngurumo zile Saba zilipotoa Sauti zao, kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya! Na iwapo huduma ya Siri za Mungu imekwisha— vipi kama hizo ni zile Siri Saba zinajitokeza?

Na kanisa dogo nyenyekevu kama letu, kwamba Mwenyezi amekuja na ameutazama unyonge wa watu Wake.

Unasema, "Vyema sidhani." Yawezekana isiwe, lakini vipi kama ndivyo ilivyo? Basi wakati umekwisha. Ulilifikiria jambo hilo? Usicheze. Yawezekana wakati umekwenda sana kuliko tunavyofikiri.

Hizo nyota zikikusanyika nyuma huko; Malaika yule akija na kusema, "Kama vile Yohana alivyopelekwa kumalizia Agano la Kale, na kuleta kutambulishwa kwa Kristo, ujumbe wako utamalizia sehemu hizo zilizolegea na utamtambulisha Masihi, kabla tu ya kuja Kwake" —ujumbe wa siku za mwisho. Angalia, yule Malaika mwenye nguvu aliapa, kwa kiapo, kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya. Sasa, sitaki kuwaweka muda mrefu sana. Hebu fikirieni jambo hili kwa dakika moja, sasa.

Sasa sikilizeni. Malaika huyu alishuka toka Mbinguni. Unaona, wale Malaika wengine Saba wa yale Makanisa Saba walikuwa wajumbe wa duniani, lakini Malaika huyu—ujumbe wote umekwisha. Malaika wa Saba anamalizia jambo lote. Na huyu Malaika anakuja, siyo duniani—Si mtu wa kutoka duniani, kama wale wajumbe wa Nyakati za Kanisa; hizo tayari zimemalizika —bali Malaika huyu analeta tangazo jingine (na malaika humaanisha mjumbe) na Yeye anashuka kutoka Mbinguni amevaa ile Nguzo ya Nuru—wingu, na upinde wa mvua juu ya kichwa Chake; na upinde wa mvua ni agano. Ilikuwa ni Kristo, huku mguu mmoja ukiwa katika nchi na

mmoja juu ya bahari, na kuapa kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya.

Je! tupo wapi, Mabwana? Mambo yote haya yanahusu nini? Ninawaulizeni ninyi.

Wale malaika wengine walikuwa wajumbe—watu wa duniani. Lakini huyu Malaika. . .hii ilisema, kwa malaika wa Kanisa la Laodikia; kwa malaika wa Kanisa la Efeso—wajumbe wa duniani. Unaona? Mwanadamu; wajumbe; manabii, na kadhalika kwa Kanisa. Lakini Huyu hakutokea duniani; alishuka kutoka Mbinguni, kwa sababu ile Siri yote imeisha kwisha. Na wakati ile Siri imekwisha yule Malaika alisema, "Hapatakuwa na wakati baada ya haya," na zile Ngurumo Saba zikatoa sauti zao.

Vipi kama ni kitu cha kutujulisha jinsi ya kuingia katika imani ya kunyakuliwa! Sio? (Tutakimbia na kuruka juu ya kuta?) Kuna jambo lililo tayari kutukia, na hii miili ya kale iliyoharibika, mipotovu, itabadilishwa? Naweza kuishi nipate kuliona, ee Bwana? Lipo karibu sana kwamba nitaliona? Hiki ndicho kizazi kile? Mabwana, ndugu zanguni, ni wakati gani? Tuko wapi?"

Hebu na tuangalie saa—kalenda—kuona tarehe tunayoishi. Israeli wako Palestina, nchi ya uenyeji wao. Ishara ya mwisho—ile Nyota yenye pembe sita ya Daudi, ya miaka elfu mbili iliyopita, (ndiyo, karibu miaka 2500 iliyopita) ile bendera ya zamani kuliko zote, inapepea. Israeli wamerudi katika nchi ya uenyeji wao. "Mtini unapochanua, kizazi hiki hakitakufa—hakitapita—hakitapita hadi mambo yote yametimia."

"Mataifa yanaanguka,
Israeli wanaamka,
Ishara ambazo manabii walitabiri.
Siku za Mataifa zimehesabiwa;
Zimekumbwa na hofu,
Rudini makwenu, enyi mliodharauliwa.

Siku ya ukombozi imekaribia.
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu.
Jazweni na Roho, huku taa zenu zimetengenezwa na zinawaka.
Inueni macho yenu, ukombozi wenu unakaribia.

Manabii wa uongo wanadanganya;
Ukweli wa Mungu wanaukana,
Kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu wetu" (Mnajua ni kweli!) . . .
"Bali tutatembea ambapo mitume wame kanyaga.
Kwani siku ya ukombozi i karibu,

Mioyo ya watu inazimia kwa hofu.
Jazweni na Roho,
Huku taa zenu zimetengenezwa na zinawaka.
Inueni macho yenu ukombozi wenu umekaribia."

Yaweza iwe karibu kuliko mnavyofikiri. Imeniogofya sana! Loo, sijafanya ya kutosha! Tuko wapi?

Hapatakuwa na wakati baada ya haya. Anatangaza kwamba wakati umekwisha. Kunatukia nini? Kunatukia nini? Ndivyo ilivyo, sasa Ndugu? Fikiri sana! Kama ndivyo ilivyo, basi ile piramidi tayari imefunikwa na zile Ngurumo Saba.

Mnakumbuka ule ujumbe wa piramidi? Ndio kifuniko. Ilifanya nini? Roho Mtakarifu alimweka kifuniko mtu binafsi na kukitia muhuri tulipoongezea kwa imani yetu: haki, na utaua, na imani, na kadhalika—tuliendelea kuongezea katika hilo mpaka tukapata vitu saba, na cha saba kilikuwa Upendo ambao ni Mungu. Hivyo ndivyo Yeye anavyomtengeneza mtu binafsi. Anamwekea kifuniko na kumtia muhuri kwa Roho Mtakatifu. Basi ikiwa ndivyo ilivyo, Yeye ana Nyakati Saba za Kanisa ambapo Yeye amekuwa na Siri Saba za Kanisa ambazo zimekwisha kupigiwa baragumu nao walizipigania kuzirudisha, na sasa Jiwe la Juu kabisa linakuja kufunika kanisa kileleni. Je! zile Ngurumo zinamaanisha jambo hilo, Ndugu zanguni? Mabwana, je! hapo ndipo tulipo?

Junie, nataka kuchukua ndoto yako. Tazama! Junior (kabla ya ile piramidi kuhubiriwa miezi kadha kabla) aliona ndoto hii. Unasema, "Ndoto ina nini?"

Nebukadreza aliota ndoto (ambayo Danieli aliifasiri) ambayo ilizungumzia mwanzo wa Wakati wa Mataifa, na lini ungeondoka. Moja imetokea sawa kabisa namna hiyo. Hakuna hata kipengele kimoja kimeshindwa.

Unaona, yale maandishi yaliyokuwa kwenye miamba; nilikuwa ninamfasiria. Walikuwa wamefurahi sana. Hiyo ni Siri ya Mungu, ambayo haijaeleweka kwa miaka mingi. Je, ingewezekana jambo hilo kuwa kitu hicho? Na halafu angalia. Kwa njia ya ajabu, tulichukua (kutoka hewani) chombo kikali ambacho kilifungua kile kifuniko, na mle ndani mlikuwa na jiwe gumu jeupe, lakini halikufasiriwa. Hapakuwa na maandishi. Sikufasiri hilo, Junior. Nililiangalia tu, na nikawaambia ndugu, "Angalieni hili," na hilo limetimizwa usiku wa leo! Walipokuwa wakichunguza hilo, nilichomoka kimya nikaelekea Magharibi. Kwa sababu gani? Labda kuelewa ile tafsiri ya lile ambalo limeandikwa kwenye kilele cha hii. Je! ndivyo ilivyo?

Na hiyo mishindo, hivi majuzi asubuhi, hiyo ambayo ilinitikisa, sana hata nikainuliwa hewani yapata urefu wa jengo hili, na lile kundi la Malaika, Malaika saba katika umbo la piramidi. Je! hizo ndizo zile Ngurumo ambazo zinakuja?

Je, ndivyo ilivyo? Hii yote imefasiriwa. Kulingana na ndoto yake, mambo yote yamekwisha. Kulingana na Neno la Mungu, Mjumbe wa Saba atamaliza . . . ujumbe wa saba utamalizika.

Na halafu zile Ngurumo Saba, naye aliona kifuniko cha juu kikivingirika, ambapo watu wengi hata hawajui kuna Muhuri Saba zitakazofunuliwa. Nimesoma vitabu vya watu wengi juu ya Ufunuo, na kamwe sijalisikia likizungumziwa. Wanaruka hilo. Lakini ninyi mmeambiwa tayari kwamba lipo! Sijui ni nini! Je, hilo ndilo? Mungu atuhurumie. Kama hilo ndilo, tuko katika saa mbaya sana.

Sasa, hebu kidogo. Angalia. Kama hivyo ndivyo, na siri imekwisha ambayo iliandikwa katika miamba hii, ninafurahi kuketi katika kanisa lenye watu wanaompenda Mungu, ambao Mungu anaweza kuwapa ndoto. Ninafurahi kuwajulisha watu hawa wanaume kwa wanawake ambao huenda kwenye kanisa la Junior, na kwenye kanisa hili, kwa la Ndugu Neville na kadhalika, kwamba wapo watu wanaoketi katika kusanyiko hili, na Biblia ilisema "Wangeota ndoto katika siku za mwisho."

Hili hapa, hebu liangalieni. Linalingana na Neno.

Bila mimi kujua cho chote kuhusu jambo hilo, mshindo ulitokea na hapa wakaja Malaika saba wakija toka Umilele. Nikasema, "Bwana, wataka nifanye nini?" Sikuambiwa. Pengine itanibidi kwenda kwanza kutafuta. Sijui. Pengine hata yawezekana isiwe hivyo, sijui. Ninajisemea tu, "Vipi kama ndivyo?" Kama ni la kimaandiko, hilo linaelekea kuwa karibu sana nalo. Sivyo?

Angalia, basi angalia, kile Kifuniko hakikufasiriwa, unaona. "Nenda Mashariki, kisha urudi." Au ni hili? Kama Malaika hawa saba walionijia katika kundi hili . . . Na nitakapokutana nanyi katika siku ya ufufuo, mtaona kwamba sidanganyi. Mungu ni Hakimu wangu.

Au hiki ni kile kilele cha pili nilichozungumza habari zake hivi majuzi. Kuna jambo fulani linalokuja kwa Kanisa? Sijui. Ningeweza kudumu katika hilo kidogo, lakini nitaendelea mbele.

Ingewezekana kwamba ile Ngurumo kuu, au yule Malaika wa Saba katika lile kundi la wale saba, kundi la kipindi cha saba, piramidi iliyoundwa katika umbo, watatu kila upande, na mmoja juu, nao walishuka toka Umilele. Je! ndivyo ilivyo: Je, hii ndiyo ile Siri ya Ngurumo ambayo itarudisha lile Jiwe kuu la Kuwekwa Juu?

Unajua, ile piramidi haikutiwa kamwe kifuniko. Lile Jiwe la Kuwekwa Juu halijaja bado. Limekataliwa. Ndivyo ilivyo, Ndugu, Dada.

Au huu ni ule mvuto wa tatu ambao Yeye aliniambia miaka mitatu au minne iliyopita.

Mvuto wa kwanza—mnakumbuka nini kilitukia? Nilijaribu kuuelezea. Alisema, “Usifanye hilo.”

Mvuto wa pili—Yeye alisema, “Usijaribu . . . ” na nilivuta kwa vyo vyote. Mnakumbuka? Ninyi nyote mnakumbuka, iko katika kanda, na kila kitu.

Halafu Yeye akasema, “Sasa kuna mvuto wa tatu unaokuja, lakini usijaribu kuuelezea.”

Mnaona jinsi nilivyoliendea hili usiku wa leo? Sijui. Lakini najisikia kuwajibika kwa Kanisa langu kusema jambo fulani. Hebu jiamlieni wenyewe.

Sasa, je, hii itakuwa ni ile Siri ambayo ingefungua, ambayo ingemleta Kristo, ilete uwezo Kanisani? Unaona tayari tumeisha . . . Tunaamini katika toba, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Tunaamini katika kumpokea Roho Mtakatifu. Tuna ishara, maajabu, miujiza, kunena kwa lugha, na yale mambo ambayo Kanisa la kwanza lilikuwa nayo. Na kwa kweli, mambo mengi zaidi yamefanyika papa hapa kuliko yaliyoandikwa katika Kitabu cha Matendo, katika kundi hili ndogo la watu, huduma hii ndogo sana yetu hapa. Na ulimwenguni mwote je? Zaidi ya yaliyoandikwa katika Kitabu cha Matendo. Aina ile ile—kufufuliwa kwa wafu. Kumbuka, kulikuwa na kama watu 3 tu waliofufuliwa kutoka kwa wafu na Yesu Kristo, nasi tuna katika rekodi (rekodi ya daktari) watano. “Kazi nizifanyazo Mimi, na nyingi kuliko hizo mtafanya.”

Najua kwamba King James inasema *kubwa zaidi,* lakini usingeweza kufanya zilizo kubwa zaidi—nyingi kuliko hizo. Alikuwa katika Mtu mmoja wakati huo, Yeye yuko katika Kanisa lote sasa. Unaona. “Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.”

Kama huu ni mvuto wa tatu, basi kuna huduma kuu iliyo mbele. Sijui. Siwezi kusema, sijui.

Angalia. Mvuto wa tatu. Hebu na tusimame katika hilo kidogo. Katika ono lile, mruko wa kwanza ulikuwa ndege wadogo wajumbe; hiyo ilikuwa hapo tulipoanza kwanza. Ilikua toka kuchukua tu mkono wa mtu . . . nanyi mnakumbuka yale Yeye aliniambia: “Kama utakuwa mwaminifu, itakuwa kwamba utajua hata siri za mioyo yao.” Ni wangapi wanaolikumbuka hilo likitangazwa toka hapa na nchini kote? Basi ilitukia? Sawa kabisa. Kisha Yeye alisema, “Usiogope, nitakuwa pamoja nawe.” Na litaendelea.

Sasa mvuto wa kwanza ulikuwa vijindege; miruko hiyo. Walikwenda kuulaki wakati; kulaki kuja kwa Bwana—ujumbe wa kwanza. Mara ya pili—siri za mioyo. Toka kwenye kuuchukua mkono wa mtu, na kusimama tu pale na kusema walilokuwa nalo. Pili ilifunua dhambi zao na kuwaambia la kutenda na kutengeneza . . . Hilo ni kweli? Basi hilo lilitimia kikamilifu

kabisa, kama tu vile Mungu alivyosema, nanyi ni mashahidi na ulimwengu pia, na vivyo hivyo kanisa.

Niliposema, "Niliona Malaika, na ilikuwa zumaradi ya moto unawaka," watu walicheka na kusema, "Billy, jirudie." Jicho la ajabu la kamera ya kisayansi lilimpiga picha Huyo. Sikuwa ninadanganya. Nilisema ukweli. Mungu aliithibitisha. Nilisema, "Kivuli kimefunika; ni kifo—cheusi; na hii ni nyeupe. Kimoja ni uzima, na kile kingine ni mauti." Hilo hapo kwenye picha nyuma huko. Kama George J. Lacy alivyosema: "Jicho la kimitambo la kamera halitapiga picha saikolojia." Mnanielewa?

Angalia, mruko mdogo wa kwanza—mkono. Wa pili ulikuwa mkuu zaidi, mweupe zaidi—hua—Roho Mtakatifu akifunua siri za moyo. Na mruko wa tatu ulikuwa Malaika! Siyo ndege, Malaika! Na huo ni wakati wa mwisho. Ni hayo tu.

Huu utakuwa ndio ule wakati Ndugu zanguni? Wakati umewadia?

Sasa, sikilizeni kwa makini, na msifasiri hili vibaya. Nataka kuwaulizeni kitu.

Hebu turudini nyuma, kidogo tu. Kanisa linajua ni ukweli.Ulimwengu wa kisayansi unajua ni kweli. Na watu wameketi hapa usiku wa leo, na wengi bado wanaishi, ambao walikuwa wamesimama pale mtoni wakati ile Sauti iliponena hilo na kusema, "Kama Yohana alivyotumwa na ujumbe wa kule kuja mara ya kwanza, vivyo hivyo huu ndio ujumbe wa pili wa kuja mara ya pili." Mnakumbuka? Na kama umekwisha, Yohana alifanya nini? Yohana ndiye aliyesema, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Huyo Ndiye."

Je saa . . . imewadia, ndugu zanguni. Sisemi imewadia. Sijui, bali nawaulizeni. Nawatakeni mfikirie. Au huu utakuwa ndio wakati itakapokuwa tena, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu;" au wakati wa Malaki 4—kujeresha mioyo ya watoto irudie imani ya baba zetu. Je, itakuwa na mshindo mkuu sana hata ita . . . ambao utatenda mambo makuu sana mpaka hata ulitayarishe Kanisa, ambalo lilikuwa ovyo ovyo, na haliwezi kuelewa Siri za Mungu, na kadhalika; waonapo huo mshindo ukienea kote, je! utageuza mioyo yao iwaelekee baba, kama vile Biblia ilivyosema ungefanya? Au huu ulikuwa ule ujumbe uliokwishapita ambao ungelitenda hilo? Sijui. Hii ndiyo ishara ya wakati wa mwisho, Mabwana? Au hii ni ishara kwamba mambo yamekwisha? Inaonekana ya kimaandiko sana kwangu. Sijui.

Palikuwa na wale Malaika. Palikuwa na mshindo, kama ngurumo, ambao ulitikisa dunia yote. Mungu ajua ninasema ukweli. Kumbuka tu, kitu fulani kiko tayari kutukia. Sijui ni kitu gani, lakini ingewezekana kuwa hiki? Sababu ya kusema hivi: jiandaeni.

Hebu na tuombe. Kuomba jinsi gani? Kuchukua mahali petu katika jeshi la waaminio Wake na tujiandae, kwani yawezekana wakati umechelewa kuliko tunavyofikiria. Mnanijua mimi, nami sijawaambia uwongo bado, kadiri nijuavyo. Na kama Samueli alivyowaambia, "Nimewaambia neno katika Jina la Bwana, ila lililotokea?" Sasa, ninawaambieni sasa, sijui hii ni nini; siwezi kusema hii ni nini. Sijui. Lakini nitaawambia ukweli—Ninaogopa. Kama ndugu yenu, nimeogopa tangu Jumamosi iliyopita.

Huenda ikawa ni wakati wa mwisho. Huenda ikawa wakati umewadia wa pinde za mvua kupita angani na tangazo toka mbinguni likisema, "Wakati umekwisha." Kama ndivyo ilivyo, hebu na tujiandae, marafiki, kumlaki Mungu wetu.

Kumekwisha wekwa chakula kingi sana sasa; hebu na tukitumie. Hebu na tukitumie sasa. Nami toka humu jukwaani, namlilia Mungu, "Bwana Yesu, nihurumie."

Nimejaribu kuishi vizuri nijuavyo. Nimejaribu kuleta jumbe, kadiri nilivyoweza, kutoka katika Neno la Mungu. Mungu ajua moyo wangu. Lakini wakati kundi lile la Malaika lilipopita kwa kasi pale ardhini, nilikufa ganzi. Hata sikuweza kuhisi kitu kwa muda mrefu. Hata nilijisikia kama . . . muda mrefu baadaye nikijaribu kutembea kwenye kile chumba, hata toka kwenye uti wangu wa mgongo, na juu na chini ya shingo yangu, nilikuwa nimekufa ganzi kabisa—hata singeweza kuhisi kwa mikono yangu. Nilipigwa na bumbuwazi mchana kutwa. Niliingia tu chumbani nikaketi chini.

Jumapili nilikuja hapa kuzungumza, nami nilijaribu kujitikisa nitokane na hilo kwa kuzungumza; Jumatatu lilikuwa pale tena. Na lipo hapa sasa. Nami sijui; sijui, Mabwana. Ninakuwa mwaminifu tu nanyi kama ndugu zangu. Sijui.

Wakati umewadia? Je! Siri yote imemalizika? Kupiga baragumu kumekwisha? Hizo hasa ndizo zile Ngurumo Saba zinazojitayarisha kutoa sauti fulani ambapo kundi lile dogo ambalo limekusanyika pamoja litapokea imani ya kunyakuliwa lipate Kunyakuliwa wakati Yeye ajapo; kwani tutabadilishwa haraka kama vile wale Malaika walivyokuja—katika dakika moja, kufumba na kufumbua macho, na tutatwaliwa pamoja na wale waliolala kumlaki Bwana hewani.

Sala yangu ni: Mungu iwapo ndivyo ilivyo, sijui Bwana, nilikuwa ninaliambia tu Kanisa. Kama ndivyo ilivyo, Bwana, andaa moyo wangu. Tutayarishe, Bwana, kwa ajili ya saa ile kuu ambayo historia yote ya wakati, manabii wote na wenye hekima wametazamia wakati huo. Bwana, sijui la kusema, ningeogopa kusema, "Usije Bwana." Naona aibu ninapoangalia na kuuona ulimwengu katika hali ile, nami sijafanya cha zaidi kuliko nilichofanya kuhusu jambo hilo; naona aibu. Kama kuna kesho, Bwana, utie upako moyo wangu; nitie upako zaidi, Baba, nipate

kutenda kila kitu niwezacho kuwaleta wengine Kwako. Mimi ni Wako.

Najisikia kama Isaya mle hekaluni siku ile alipoona wale Malaika wakiruka huku na huko, na mabawa yakifunika nyuso zao na miguu yao, wakiruka kwa mbawa—“Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu.” Loo, jinsi huyo nabii kijana alivyoogopeshwa! Alianza kukua kidogo; naye alipoona hilo, ingawa ameona maono alipiga makelele, “Ole wangu.”

Baba, labda nimejisikia kwa namna fulani kama hivyo, nilipoona hao Malaika usiku wa juzi—au hivi majuzi asubuhi, hasa. Ole wangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninaishi katikati ya watu wachafu.

Na Baba, nitakase; mimi hapa, nitume, Bwana, cho chote kile . . . ninaposimama kwenye mimbara hii ambapo nimekuwa kwa miaka thelathini. Kama kuna jambo fulani, Bwana, ambalo Wewe unanitaka nitende, mimi hapa. Niko tayari, Bwana. Lakini hebu nipate neema machoni Pako, kwa unyenyekevu, ninaomba.

Naliombea kundi hili dogo, ambalo Roho Mtakatifu amenifanya mimi kuwa mwangalizi wake, kuwalisha. Nami nimetenda yote yale nijuayo jinsi ya kutenda, Bwana, kuwalisha Mkate wa Uzima. Kama katika ono lile, miaka mingi iliyopita, ambapo pazia lile kuu lilikuwa huko Magharibi, na mlima wa Mkate wa Uzima. Kitabu kile kidogo, *Sikuyaasi yale Maono ya Mbinguni,* na hapa yote yametimia, yamefunuliwa mbele ya nyuso zetu.

Wewe ni Mungu, na hakuna mwingine ila Wewe. Tupokee Bwana; tusamehe dhambi zetu. Ninatubu kwa kutokuamini kwangu kwote, kwa uovu wangu wote. Nasihi juu ya madhabahu ya Mungu.

Ninapokuja usiku wa leo pamoja na kanisa hili dogo mbele yangu, kwa imani tunaondoka kwenye jengo hili katika kunyakuliwa, tukiketi pamoja katika Ulimwengu wa roho kuzunguka Kiti cha Enzi cha Mungu. Mioyo yetu imepashwa moto mara nyingi katika mambo yale tuliyokuona Wewe ukitenda na ukifunua Siri Zako kwetu. Lakini, Bwana, usiku wa leo nimechoka kabisa. Ole wangu. Kama vile Yakobo, alipoona Malaika wale wakishuka na kupanda ngazi, alisema, “Mahali hapa panatisha, bila shaka hapa ni Nyumba ya Mungu.” Basi Bethel ikajengwa hapo.

Mungu, watu hawaelewi kwamba . . . Wanafikiria itakuwa furaha kuu, bali Bwana, ni jambo la kuchosha, na la kutisha jinsi gani, kwa binadamu kuja kwenye uwepo wa Kiumbe kikuu chenye uwezo cha Mbinguni.

Naomba msamaha kwa kanisa langu dogo hapa, ambako Wewe umenituma kulielekeza na kuliongoza. Wabariki, Bwana. Nimetenda kulingana na yale maono na ndoto na kadhalika

vimesema kadiri nijuavyo mimi. Nimehifadhi chakula chote, vizuri nijuavyo, kwa ajili yao, Bwana. Hata iwe nini, Bwana, sisi tu Wako. Twajitoa mikononi Mwako, Bwana. Tuhurumie, tusamehe, na tujalie kuwa mashahidi Wako maadamu tuko duniani. Ndipo, maisha haya yakomapo, tupokee katika Ufalme Wako. Kwani twaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

Kila mmoja wenu, safisha moyo wako wote. Weka kando kila kitu, kila mzigo. Uondoe kwako. Usiache jambo lolote likutie wasiwasi. Usiogope. Hakuna cha kuogopa. Kama Yesu yuaja, ni. . .ni wakati ambapo ulimwengu mzima umeuugulia na kuulilia. Kama ni kitu kinachokuja sasa, kwa kuja kupya—kuja kupya kwa kipawa kipya au jambo fulani, litakuwa jambo zuri sana. Iwapo wakati umewadia wa Kanisa kufunuliwa zile Ngurumo Saba (jinsi ya kuondoka) sijui. Nimetamka tu yale niliyoona.

Loo jamani, wakati wa jinsi gani! Ni mzito na wa mawazo mazito. Na kama wakati wa kuondoka kwangu umewadia, mimi ni Wako, Bwana. Mimi ni Wako. Utakapomaliza, njoo, Bwana Yesu. Hata iwe wapi au iwe wakati gani, mimi ni Wake. Sisemi ninatamani kuondoka; sitamani. Nina familia ya kulea; nina Injili ya kuhubiri, lakini hilo ni sawasawa na mapenzi Yake, sio yangu. Hayo ni mapenzi Yake, sijui. Ninawaambia tu ni nini. Hata liwe nini—Mungu atalitimiza. Bali, nawaambieni yale niliyoona na yaliyotukia. Yalivyomaanisha, sijui; lakini Mabwana, je! yawezekana kuwa huu ndio mwisho?

Watu wale wapo sasa—wale watu sita, ambao walikuwa na ndoto zile. Je! si ni ajabu kwamba hapakuwepo na saba? Ni ajabu mno kwamba sita zilifuatana moja kwa moja, mara likatokea lile ono. Wale watu wapo hapa. Ndugu Jackson, hapa alikuwa mmoja; mwingine Ndugu Parnell; mwingine Dada Collins; mwingine Dada Steffy; mwingine Ndugu Roberson; na mwingine Ndugu Beeler; na Baba wa Mbinguni anajua hapakuwa na nyingine zaidi inayohusiana na hilo. Mwishoni mwa ile ya saba (ambayo ilikuwa Dada Steffy) mara lile ono likatokea.

Mnaona? Mnaona kwa nini ninaondoka? Mnaona kwa nini inanipasa kwenda? Lazima nifanye hivyo. Enyi marafiki, msiniangalie. Mimi ni ndugu yenu. Msinijali mimi, kwa sababu mimi ni binadamu tu. Sina budi kufa kama mtu mwingine ye yote. Msinisikilize mimi, bali sikilizeni kile nilichosema. Nilichosema ni ujumbe. Msimjali mjumbe kamwe; angalieni ujumbe. Kazeni macho yenu, si juu ya mjumbe, lakini juu ya ujumbe—kile ulichosema. Hilo ndilo jambo la kuangalia; na Mungu atusaidie, ndilo ombi langu.

Sasa, sikutaka kuja kuwaambieni hili, lakini nisingaliwaficha jambo. Sasa, kadiri nijuavyo. . .hebu niwaambieni. . .kadiri nijuavyo, nitaondoka katika siku mbili

au tatu zijazo (Jumatano asubuhi) kwenda Tucson. Siendi Tucson kuhubiri; siendi huko kuhubiri. Naenda Tucson kuwaingiza familia yangu shuleni, halafu niwe mtembezi. Naenda Phoenix kufanya ule mfululizo wa mikutano midogo, ambayo labda itakuwa jumbe ndogo hapa na pale; nao labda, nafikiri wananitaka nihubiri katika mkutano usiku mmoja. Hawakusema kamwe cho chote juu yake, walisema tu nitakuwepo pale. Unaona, hilo halionekani kuwa zuri sana kwangu. Nina neno, BWANA ASEMA HIVI kwa Ndugu Shekarian, pia. Sijui atafanya nini kuhusu jambo hilo, lakini nina neno la kumwambia. Sijui atafanya nini; ni juu yake.

Mmechunguza ile nakala ya mwisho ya "Sauti"? Haipaswi kuwa madhehebu, lakini walitangaza kanuni yao ya imani. Madhehebu, basi nikaondoka, niko nje ya jambo kama hilo.

Sasa, nadhani Ndugu Arganbright na Ndugu Role, mjumbe wa serikali huko Washington chini ya marais saba, apaswa kuwa Afrika. Na Ndugu Role, mimi, na Ndugu Arganbright tutazuru Afrika mara moja kwa ajili ya mikutano—huko Afrika ya Kusini na Tanganyika pamoja na Ndugu Boze, na kuendelea huko chini na labda kupanda kwenda Australia na kupitia njia hiyo tukirudi, kama Bwana hafanyi jambo la tofauti. Lakini kabla ya kwenda, nitarudi hapa.

Basi nitakaporudi toka huko, kama Bwana hakunena nami kwa njia nyingine, nitachukua familia na kusogea kule juu karibu na Anchorage, Alaska. Huku ni Kusini-Magharibi, kule itakuwa Kaskazini-Magharibi. Halafu, niwaache wakae huko majira ya kiangazi, wakati ni joto sana chini huko Tucson mpaka itakuunguza ngozi. Sidhani wangeweza kulistahimili. Watakuwa na hamu ya nyumbani sana na kuvunjika moyo. Hatuuzi mahali hapo. Patabaki hapo na fanicha ikiwamo nyumbani. Sijui la kufanya.

Basi, wakati wa majira ya joto ukiisha, kama Bwana akipenda, nataka kuondoka Alaska, na kushuka kwenda kama Denver—Magharibi ya Kati. Kusini-Magharibi, Kaskazini-Magharibi, Magharibi ya Kati, nikilia, "Ee Bwana, Wewe wataka nifanye nini."

Wakati ule ule, kila ujumbe, kadiri nijuavyo, utahubiriwa papa hapa, maskani hii. Hapa ndipo kanda zitakapokuwa; hapa ndipo penye makao makuu, nami sikusudii kukaa Magharibi na familia yangu. Nitatafuta hata nione ambalo Mungu ananitaka nifanye. Iwapo mwaka huu haulitatui, basi mwaka ujao, bila ya maji au chakula, nitatembea nyikani, nami nitangojea mpaka Yeye atakaponiita. Siwezi kuendelea hivi. Yakubidi ukate tamaa. Yakubidi ufikie mahali ambapo unataka kujua Mapenzi ya Mungu, na wawezaje kutenda Mapenzi hayo, kama huyajui yale atakayo? Ninahojihoji kwa sababu ya chanzo cha lile ono kwa yale mliyoona; naenda huku na huko kama mmishenari

na uinjilisti mpaka mwito ule uje. Mnakumbuka lile la kwanza wakati tulipoweka jiwe la msingi? “Fanya kazi ya mhubiri wa Injili,” Yeye akasema. Haikusema u mwinjilisti, lakini fanya kazi yake; labda mpaka wakati ufike wa jambo jingine, badiliko jingine la kazi. Yaweza iwe jambo tofauti. Sijui.

Mnampenda Yeye? Iweni na hakika kabisa ya jambo hilo. Iweni na hakika kabisa ya jambo hilo. Hao wampendao Bwana.

“Wao wamngojeao Bwana,
Watapata nguvu mpya.
Watapanda juu kwa mbawa kama tai,
Watapiga mbio wala hawatachoka;
Watatembea kwa miguu wala hawatachoka.
Ee nifundishe mimi Bwana, nifundishe Bwana
kungojea.”

Ninampenda, na ninajua nanyi pia mwampenda.

Sasa, kesho usiku. . . Nafikiri nimeliweka wazi sana. Sivyo? Wazi niwezavyo. Hayo ndiyo yote nijuayo. Hayo ndiyo yote nijuayo kusema. Na iwapo limefunuliwa kwangu kuhusu jambo fulani, upesi sana nitawaambia. Najua mnataka kujua. Mimi ninataka kujua. Sijui inamaanishwa nini; sijui naenda wapi; sijui litakalotukia. Nina tu. . . Jambo tu nilijualo, ninaenda kwa neema ya Mungu. Ndipo basi Yeye ataniambia nitakapofika pale, labda. Lakini sehemu yangu sasa ni, nenda. Basi huenda nisiwepo huko majuma mawili hadi nitakapokuwa mahali pengine, na huenda nikarudi hapa. Hilo ni kweli. Sijui lakini mimi. . . Ono lile lilikuwa na mke wangu na watoto wangu ndani yake, na jambo lenyewe hasa ni kwamba—nilikuwa katika gari lenye turubai na mara tu nilipoingia pale, palikuwa. . . Nilikuwa katika gari langu kubwa. Na hivyo ndivyo tunavyoondoka katika siku chache—bila kujua ambako tunaenda, bila kujua tutakalofanya tutakapofika kule. Tunaenda tu.

Mungu ni wa ajabu kwetu kwa sababu njia Zake hazitafutiki. Anataka utii.

“Unakwenda wapi?”

“Hiyo si kazi yako, endelea tu kwenda.”

“Unanitaka nifanye nini, Bwana?”

“Hicho si kitu kwako, Wewe nifuate. Endelea tu kutembea.”

“Nitasimama wapi?”

Hilo lakupasaje? Endelea tu kutembea.” Kwa hiyo mimi hapa naenda. Katika Jina la Yesu Kristo.

“Nampenda,
Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda . . . (Yeye ni uzima wangu) . . .
Nampenda . . . (Yote niliyoishia) . . .
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu mtini Kalvari."

Je! Mabwana, Huu Ndio Ule Wakati?

Na wakati tunauimba tena, peana mikono na mtu fulani aliye karibu nasi. Sema, Ndugu au Dada, niombee nami nitakuombea.

Hii Ndiyo Ishara Ya Mwisho, Bwana? SWA62-1230E
(Is This The Sign Of The End, Sir?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 30 Desemba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org